# KWA NINI BETHLEHEMU MDOGO

Ni vyema kuwa hapa asubuhi ya leo. Na sasa ninaamini tunaenda kuwa na uimbaji spesheli, Ndugu Williams alikuwa akiniambia, na mtu fulani kutoka kanisani mwake. [Dada mmoja anaimba, *Kijaze Kikombe Changu, Bwana*—Mh.] Hicho ndicho kilichotuleta hapa asubuhi ya leo, kuinua vikombe vyetu, "Kijaze, Bwana." Huu ndio wakati pekee ambao tutakuwa na fursa kuomba jambo hili. Kutakuja wakati ambapo tutakuwa upande ule mwingine na wakati huo hatutakuwa na fursa hiyo. Kwa hiyo wakati tukiwa nayo, na tukiwa na akili timamu, nafikiri mojawapo ya mambo ya maana kuliko yote mtu yeyote awezalo kufanya wakati Mungu ametupa fursa ya kufanya hivyo, ni kulifanya, kuvifanya vikombe vyetu vijazwe sasa na upendo na rehema Zake.

2 Yupo mmoja aliyeketi nasi muda mrefu uliopita, sio muda mrefu sana uliopita, hata hivyo, naye ameaga dunia. Na ni huzuni kubwa mioyoni mwetu kwa ajili ya Ndugu Williams. Ni Ndugu Williams, rais wa tawi letu hapa, baba yake. Baba yako alikuwa na umri gani, Ndugu Williams? Themanini na nane. Huo ungekuwa yapata miaka kumi na minane, nadhani, zaidi ya ninii—ninii . . . la, ingekuwa, naam, miaka kumi na minane zaidi ya muda ulioahidiwa. Mtu hodari. Haujakuwa muda mrefu sana tangu, tulipoketi kwenye mkutano, nikamwambia, na si kumkosea heshima Ndugu Williams, nikassema, "Unaonekana mdogo wa umri kuliko mwanao, Carl." Inaenda tu kuonyesha kwamba tupo hapa leo na kesho hatupo hapa. Hatujui wakati huo ujapo, unapokuja, bali tunajua unakuja. Nilikuwa nikiwaza, lakini uhai ni kitu kikuu, ndivyo ulivyo, uhai ni fursa.

3 Ndio kwanza tuwe na msiba mkubwa, wa mmoja aliyekuja kanisani mwetu kwa muda mrefu sana, kutoka Chicago, aliuawa hivi majuzi akija nyumbani, mama. Alikuwa karibu, nadhani karibu miaka sabini, na yeye na mume wake wakisafiri moja kwa moja na huko Kansas, Missouri, mmoja, dhoruba kali ya theluji ikienenda. Mtu akiendesha motokaa, motokaa ikapoteza mwelekeo, shingo yake ikavunjika papo hapo. Nasi hatujui ni wakati gani hili linapokuja. Wakati mimi . . . walinipigia simu kuniambia kuhusu hilo ndipo nikawapigia simu watoto wote kote katika taifa, nikiwaambia. Maana, nikiwa kama, mchungaji wao, ni mimi niliyepaswa kuwajulisha. Nikiwazia jinsi tunavyoweza kuenda upesi, na halafu hapo kulikuwapo na kasha la peremende limewekwa mbele yangu alilonitengenezea yapata juma moja lililopita, na akanipa. Kuona tu jinsi tunavyoweza kutwaliwa upesi. Lakini, ikiwa huo, ikiwa uhai huu pekee ulikuwa ndio mahali tulio na matumaini yetu, tungekuwa ni watu wenye mashaka. Ayubu alisema, katika

mlango wa 14, "Loo, laiti Wewe ungenificha kaburini na kuniweka mahali pa siri."

4 Je! umewahi kutambua jinsi maumbile humshuhudia Mungu? Tunaona miti, majani huanguka kutoka kwenye miti, na uhai katika mti huingia chini ardhini, kama kaburini, na hukaa huko mpaka ghadhabu ya baridi kali imepita, kisha unarudi tena, ukileta uhai mpya. Ni ushuhuda kwamba tunaishi tena. Jua huchomoza asubuhi, mtoto mchanga tu, ni hafifu; baada ya kitambo kidogo ni wakati huu yuko shuleni, shule ya sekondari ya juu; halafu wakati wa adhuhuri yuko kwenye nguvu zake; kisha alasiri anaanza kugeukia upande ule mwingine; ndipo jioni anakuwa mnyonge tena na anakufa. Lakini, huo sio mwisho wa jua, huchomoza tena asubuhi inayofuata kushuhudia kizazi kingine, kwamba kuna uhai, kifo, kuzikwa, na kufufuka.

5 Hata maumbile kila mahali hunena habari Zake. Nayo maumbile ni ushuhuda mkuu kwa njia nyingine, hiyo ni kusema, kwamba hatuwezi kuwa na Uhai huu wa ufufuo isipokuwa utumikie kusudi la Mungu. Sasa, mbegu ikipandwa, na hiyo mbegu imerutubishwa, huzaa ua jipya. Lakini ikiwa haijarutubishwa, haitazaa ua jipya, ikiwa haitumikii kusudi la Mungu. Hata hivyo, si tu kwamba ni ua basi linafufuka, kwa sababu linatumikia kusudi la Mungu. Hiyo ndiyo sababu jua huchomoza, ni kwa sababu linatumikia kusudi la Mungu. Nasi tunafufuka tukitumikia kusudi la Mungu.

6 Ninaamini kwamba Ndugu Williams alitumikia kusudi la Mungu maishani, baba halisi. Pia ninamwona mwenzi wake mpendwa, Bibi Williams, ameketi hapa. Mume halisi, hilo ni moja ya makusudi ya Mungu. Baba, moja ya makusudi ya Mungu. Naye alirutubishwa kwa Mungu, na Roho Mtakatifu, kusudi kuu la Mungu. Kwa hiyo, kusema kwamba Ndugu Williams hatafufuka na kuwa pamoja nasi tena, ingetubidi kusema kwamba hakuna—hakuna kwenda chini kwa utomvu, hakuna kuchomoka kwa jua. Kila kitu huzungumzia kufufuka kwake tena, kuwa pamoja nasi tena, kila kitu. Kwanza, jua, maua, maumbile, uhai wa mimea, kila kitu kinanena habari zake. Halafu Neno la Mungu hunena kwa ajili yake. Na, kando na hayo, imani ile ile iliyoko mioyoni mwetu hudunda kwamba tutamwona tena. Mungu aipumzishe nafsi yake. Kama tu heshima kidogo kwake yeye ambaye aliketi nasi wakati mmoja, hebu tusimame kwa miguu yetu kwa dakika moja.

7 Baba wa Mbinguni, hatujawahi kuandaa mkutano kama huu kusudi tu kuonekana au kusikika. Tumekuja pamoja kila mara, kwa ajili ya kumsifu Mwana Wako, Yesu Kristo, na kutoa ushuhuda kwa wale wasio na Yeye, ili waweze kumpata. Sisi, mioyo yetu imejaa huruma kwa ajili ya wale walioachwa nyuma kutokana na kuondoka kwa ndugu yetu, yule aliyeketi nasi si muda mrefu uliopita, ambaye mara nyingi ameketi moja kwa moja kwenye tawi lili hili. Lakini tunaamini kwamba

Wewe ulimjalia kuishi maisha mazuri, makamilifu kwa njia zote, nayo nafsi yake iko pamoja na Wewe leo. Mpumzishe, Ee Mungu, hata siku ile ambapo tutamwona tena. Mbariki mwanawe hapa, watoto wake wengine, mke wake mpendwa, na wale waliompenda, na hiyo ni sisi sote, Baba. Pia jalia tutambue hili, kwamba sisi pia tu dhaifu na hatuna budi kuondoka siku moja, kwa hiyo hebu tujitayarishe kwa saa hiyo kuu. Na iwapo kuna wengine hapa asubuhi ya leo ambao hawajajitayarisha kwa ajili ya tukio lili hili, jalia hii iwe ndiyo siku ambapo watasema "ndiyo" kwa Bwana Yesu, na pia warutubishwe Kwake na Roho Mtakatifu. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina. Ketini.

8 Sasa, tunataka kutangaza ma—matangazo machache. Mke wangu anayeketi pale nyuma asubuhi ya leo, nilimwambia, nikasema, "Mpenzi, sitakuwa kwenye kiamshakinywa. . . " Ilitubidi kwenda sehemu ya chini ya mji na kufanya mambo fulani. Ndipo nikasema, "Nitatoka saa nne." Akanitazama. Nikasema, "Nisipotoka kufikia saa nne, nitakununulia magauni matatu mapya utakayojichagulia." Kwa hiyo ni—ninajua kinachoenda kutukia, nina deni ya magauni matatu hivi sasa, maana ni saa nne kasoro dakika ishirini sasa. Lakini nitajaribu kuharakisha upesi iwezekanavyo.

9 Tuna furaha kuwa hapa Yeriko pamoja na nyinyi ndugu asubuhi ya leo, na tunawaalikeni, Jumatatu usiku, Yerusalemu, huko Tucson, kwenye dhifa kule chini. Mnaona, Phoenix uko kwenye bonde, kama Yeriko. Tucson, ninakoishi, uko mlimani, huo ni—huo ni Yerusalemu. Uko wapi, Tony? Mbona mtu fulani asiseme "amina" mahali fulani hapa. Hapa, sasa niko kwenye mtego, Tony hata hakuonekana. Vema, kesho, ama Jumatatu usiku, ni dhifa huko—huko Tucson, na hakika tungefurahia kama mko karibu huko, mngeingia na kutuona. Somo langu usiku huo, Bwana akipenda, ni, *Tumeiona Nyota Yake Mashariki Na Tumekuja Kumsujudia*.

10 Na sasa tarehe kumi na tisa mwezi huu, au mwezi ujao, hasa, tarehe kumi na tisa ya—ya Januari, ninaanzisha uamsho hapa, papa hapa katika chumba hiki, hapa katika Hoteli ya Ramada, na tarehe kumi na tisa, ishirini, na ishirini na moja. Ndipo basi tarehe ishirini na mbili, naamini, inaanza ninii. . . tarehe ishirini na tatu, nina siku nne usiku hapa, na kama uamsho. Wengi wenu ndugu wahudumu, hakika tuna furaha kuwa pamoja nanyi asubuhi ya leo, na sisi tunawaalika kwa moyo mkunjufu kuwaleta watu wenu. Wale hasa, ambao, ambao mnajua hapa mjini ambao hawamjui Yesu kama Mwokozi wao. Halafu basi, pili, kwa wale walio wagonjwa na—na wanaamini kwamba Mungu huyajibu maombi, tunakusudia kuwaombea wagonjwa kwenye wakati huu kabla ya Mkutano mkuu wa Kitaifa utakaofanyika hapa kuanzia tarehe ishirini na mbili. Nami nina hakika mnataka kusikia huo, kwa sababu kuna

wahubiri wengi mashuhuri wanaokuja, na nina hakika mtakuwa na wakati mzuri.

11 Sasa, asubuhi ya leo, nimewazia kuhusu kuzungumza hapa kwenye tawi hili, ambapo Phoenix daima pamekuwa ni mahali moyoni mwangu. Ninapenda Phoenix. Nilikuwa hapa nilipokuwa ni mvulana mdogo, hapa nje Wickenburg hapa juu. Na kuishi hapa kwenye Barabara ya kumi na sita na Henshaw. Ilikuwa jangwa wakati huo. Bali ninaona iko moja kwa moja katika mji mkuu, na, vema, hasa katikati ya mji. Inaenda kuonyesha kwamba kuna wakati wa mabadiliko, mabadiliko. Lakini lipo jambo moja ninalotaka kuzungumzia asubuhi ya leo, ni Yule asiyebadilika, huyo ni Mungu. Mungu, katika mpango Wake, Neno Lake, Hilo halibadiliki kamwe. Nyakati hubadilika, watu hubadilika, mifumo hubadilika. Bali Mungu habadiliki kamwe, Yeye anabaki yeye yule.

12 Pia niliwazia, kwa kuwa tulikuwa tunakaribia wakati wa Krismasi, kwamba tungeninii. . .labda ningezungumza juu ya u—ujumbe wa Krismasi. Na sasa kama mna Biblia zenu, na mnataka kusoma, wakati mwingine watu husoma, nyuma ya wainjilisti ama mhubiri, ninataka kusoma kutoka kwenye Injili ya Mathayo Mtakatifu, mlango wa pili, kwa ajili ya fungu la Neno.

> *Yesu alipozaliwa katika Bethlehemu ya Uyahudi zamani za mfalme Herode, tazama, mamajusi wa mashariki walifika Yerusalemu,*
>
> *Wakisema, Yuko wapi yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi? Kwa maana tuliiona nyota yake mashariki, nasi tumekuja kumsujudia.*
>
> *Basi mfalme Herode. . .aliposikia hayo, alifadhaika, na Yerusalemu pia pamoja naye.*
>
> *Akakusanya wakuu wa makuhani wote na waandishi wa watu, akatafuta habari. . .kwao, Kristo azaliwa wapi?*
>
> *. . .wakamwambia, Katika Bethlehemu ya Uyahudi; kwa maana ndivyo ilivyoandikwa na* manabii,
>
> *Nawe Bethlehemu, katika nchi ya Yuda, hu mdogo kamwe katika majumbe wa Yuda; bali kwako atatoka Mtawala, atakayewachunga watu wangu Israeli.*

13 Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa Neno Lake. Na sasa nikiwa na muhtasari hapa, na Maandiko fulani ya kurejea. Ningetaka kuwa na usikivu wenu mkamilifu kwa muda mfupi juu ya somo la: *Kwa Nini Bethlehemu Mdogo*.

14 Mnajua, kwenye Krismasi, ninafikiri sisi sote, wengi wetu, nisingesema sote, bali wengi wetu hupoteza thamani halisi ya Krismasi. Kama ninavyotambua hapa nje, hata miti ya mitende imepambwa; na huko mashariki daima ni msonobari,

ama mti wenye majani mwaka mzima. Na miezi, au majuma, hasa, huenda ni mwezi mmoja ama majuma sita kabla ya Krismasi kuanza, daima ni mapambo na—na ninii mashuhuri . . . Waliifanya ya kibiashara badala ya kile inachomaanisha hasa.

15 Siamini kwamba Kristo alizaliwa tarehe ishirini na tano Desemba. Si—siamini hiyo hata kidogo. Isingewezekana kwa mambo hayo kutendeka. Milima ya Uyahudi ina theluji zaidi, mbona, theluji inafika kiunoni katika mwezi wa—wa Desemba, huko katika Uyahudi. Lakini tunatambua katika kusoma historia, Kristo labda alizaliwa katika majira ya kuchipua, yapata labda Aprili ama Mei, mahali kama hapo. Lakini wakati ilipobadilishwa, hii, waliileta, wakati Ukristo ulipobadilishwa kuwa Uroma, walifanya siku ya kuzaliwa ya mungu-jua, ambayo ilikuwa ni jua kwenye tarehe ishirini na tano, kuanzia tarehe ishirini na moja hadi ishirini na tano ya Desemba, jua likitua, ni kama, karibu haibadiliki hata kidogo. Halafu basi hiyo ilikuwa ni siku ya kuzaliwa kwa mungu-jua, kwa hiyo wakaibadilisha kuwa Mwana wa Mungu.

16 Lakini, kumbukeni, siku yoyote hiyo iwezayo kuwa, bado hatuondoi utakatifu wa kile inachopaswa kuwa. Ambapo Shetani ametunyang’anya hii, ameifanya biashara kubwa, na Santa Klaus akanyakua ibada yote. Nayo imekuwa si—siku kama Pasaka, kama vile watoto wa sungura na mabata wenye rangi ya waridi. Na—na basi hayo yana uhusiano gani na Pasaka? Hayo yana uhusiano gani na kufufuka kwa Kristo?

17 Ni kama tu ulimwengu leo hii, hao, watoto barabarani wanaweza kukuambia mengi kuhusu Davey Crockett kuliko wanavyoweza kuhusu Yesu Kristo. Wanaweza kukuambia mengi zaidi kuhusu haramia fulani, mhalifu fulani wa siku zilizopita, kuliko wanavyoweza kumhusu Mfalme wa Uzima ambaye—ambaye alizaliwa miaka elfu moja mia tisa iliyopita. Lakini hiyo haiondoi kitu halisi kutoka kwetu sisi Wakristo.

18 Mnaona, daima nuru huangaza vizuri zaidi katika giza. Radi iliyogawanyika kwenye anga zenye mawingu na giza usiku, inaonyesha kwamba kunaweza kukawa na nuru kwenye giza. Na wakati nuru ikiangaza, huoni . . . Kama jua linawaka, huhitaji taa sana. Bali giza zaidi, ndivyo nuru inakuwa ndogo zaidi, nayo itaangaza zaidi kwenye giza. Kukiwa giza zaidi, ni bora, inajionyesha vizuri zaidi. Na hiyo karibu . . . Sisi Wakristo tunapaswa kuwa tukishuhudia utukufu wa Mungu kutupatia Mwana Wake. Krismasi hii inapaswa kuwa ni kitu mashuhuri. Sisi Wakristo tunapaswa . . . Haijalishi ni kiasi gani inavyoonekana, itaifanya kuangaza vizuri zaidi. Ulimwengu wote umejaa mapambo. Tunaye Kristo, na hiyo ndiyo tunayopaswa kuwa tukiiacha iangaze katika wakati huu wenye giza tunaoishi sasa.

19 Tunawazia jinsi ambavyo Mungu hufanya mambo kwa njia zisizo za kawaida, kwa sababu Yeye Mwenyewe si wa kawaida. Mungu si wa kawaida. Yeye ni—Yeye ni wa Kimbinguni, Asiye na kikomo, kwetu tulio na kikomo. Kwa hiyo, chochote afanyacho, katika uwezo wake, si cha kawaida. Naye Mungu ni m—mkuu sana, hata anachukua vitu visivyotambulishwa vya duniani kujitambulisha Mwenyewe kwavyo.

20 Tunatambua hapa katika somo langu, la *Kwa Nini Bethlehemu Mdogo*, ule mdogo zaidi wa Uyahudi wote, majumbe wa miji mingine ya Uyahudi, ni kwa nini Mungu alichagua kumtuma Mwana Wake mahali hapo? Hilo ndilo tunalotaka kuzungumzia. Mungu akivichukua vitu vya ulimwengu, ninaamini Maandiko yanasema, "Kwa upumbavu wa kuhubiri, ilimpendeza Mungu kuchukua vitu visivyotambulishwa." Kile tunachokifanya kikuu, Mungu anakiita upumbavu. Kile tunachowekea utukufu mwingi, Mungu anasema ha—ha—hakina uzuri wowote. Na kile tunachodhania kuwa hakina uzuri, Mungu hukitukuza.

21 Nilikuwa nikiwaza kuhusu kabla tu ya kuzaliwa kwa Bwana wetu, wakati manabii wote, na kadhalika, walikuwa wamenena kuhusu mtangulizi ajaye, "jinsi kila mlima utashushwa na mabonde kuinuliwa, nayo milima itaruka kama wanakondoo, na matawi kupiga makofi yao." Na ilikuwa ni m—mhudumu, nabii jina lake Yohana, alikuja kutoka nyikani, si hata kutoka kwenye shule ya kithiolojia, masharafa yamejaa usoni mwake, na kipande cha ngozi ya kondoo, si aliyevaa mavazi ya kikasisi, ajitokeze na kutangaza, "Ufalme wa Mungu umekaribia!" Na ilikuwa vigumu kwa watu kuelewa mtu wa namna hiyo akija, bila utambulisho wowote wa m—mfumo wowote, chochote ambacho alikuwa mwanachama wake, kadi yoyote ya ushirika, ama dhehebu lolote lililokuwa linamwunga mkono. U—Ujumbe ulikuwa mkuu sana, asingemchukua mtu, Mungu alimfunza huko nje nyikani. Ujumbe wake haukuwa kwenye mi—misingi fulani ya kithiolojia. Alinena kuhusu nyoka na mashoka na miti, na hayo ndiyo aliyozoea, maumbile, kuona, jinsi yalivyofanya. Basi hiyo ndiyo nji—njia aliyoendea. Si kama kasisi, bali kama m—mtu wa maumbile.

22 Na ilikuwa vigumu kwa watu kumwelewa. Hata hakuwa na mimbara, na labda hakukaribishwa katika yoyote, lakini alihubiri kwenye kingo za Yordani, labda akisimama katika matope karibu kumfikia magotini. Bali watu walijitokeza kuusikia, wale waliokuwa waaminifu moyoni. Walitaka kusikia kwa sababu lilikuwa ni jambo tofauti, lilikuwa na sauti ya Kweli ndani yake.

23 Leo hii tunapaswa kuwa tu kwenye katika kukaribia kuzaliwa kwa Kristo; Ujumbe wetu, unapaswa kuwa na sauti ya Kweli ndani yake itakayofanya watu kuwa na kiu ya kumpata Yeye.

24 Mungu alimchukua mtu huyo rahisi, asiye na elimu, hakuwa shuleni hata siku moja, na hata hivyo kasema alikuwa mkuu kuliko wote miongoni mwa manabii wote waliowahi kuishi, kwa sababu Mungu hujitambulisha Mwenyewe katika vitu visivyotambulishwa.

25 Wakati Yesu alipowachagua wanafunzi Wake, ilikuwa hivyo. Kulikuwa na wanaume wengi waliohitimu zaidi kwa kazi hiyo kuliko hao wanafunzi, walikuwa ni makasisi, Yeye hakumwita hata mmoja. Kulikuwa na makasisi katika siku hizo, watu mashuhuri, makuhani, watu wa elimu, watu wenye sifa, bali Yeye hakuwaita. Aliwachukua wavua samaki na watoza ushuru, na kadhalika, ku—kuupeleka Ujumbe Wake. Yeye daima hufanya hivyo.

26 Katika siku za Nuhu, alimchagua mkulima, mkulima tu wa kawaida, kutangaza maangamizi ya wakati huo. Mkulima tu wa kawaida, si kasisi, mkulima tu! Katika siku za Nuhu, Yeye alichukua ninii—ninii . . . Samahani.

27 Siku za Musa, alimchukua mtumwa mtoro, si kasisi. Na Yeye alimwacha atoke nje mpaka Yeye aliporidhika, huko nje nyuma ya jangwa, na kupoteza elimu yake, na akaonekana kwake katika kichaka kilichowaka moto, na kumtuma huko chini akiwa na fimbo iliyopinda mkononi mwake, kuchukua mamlaka juu ya taifa ambalo lilikuwa . . . ambalo alikuwa amelitoroka.

28 Unaona, Mungu huchukua vitu rahisi ili kujitambulisha Mwenyewe kuvipitia. Unaona, kuchukua ninii Yake, ni Neno Lake tu. Aliufanya ulimwengu kutokana na vitu ambavyo—ambavyo vina . . . havijaonekana.

29 Siku chache zilizopita nilikuwa kwenye Ukumbi wa Morris, moja ya miamsho yetu mikubwa ya New York, na nilikuwa nikisikiliza hotuba kuhusu Einstein akizungumza kuhusu hili kundi la nyota, ambayo alisema inahitaji miaka milioni mia moja na hamsini ya—ya wakati wa nuru, kulifikia, na miaka milioni mia moja na hamsini kurudi. Halafu basi, hebu wazia, miaka milioni mia moja na hamsini ya nuru, hiyo ingekuwa miaka milioni mia tatu ya nuru. Ndipo basi uliporudi huku, ungekuwa tu umeenda miaka hamsini. Wazia, mbona, jinsi nuru inavyosafiri upesi, maili mia moja na themanini na sita elfu kwa dakika moja, na uwazie ni bilioni ngapi na trilioni za miaka ambayo ingehitajika kwenda huko na kurudi. Mia moja na ishirini . . . miaka milioni mia tatu ya nuru. Na hiyo tu ni kufikia kundi la nyota katika galaksi ambayo Mungu alipulizia tu kutoka mikononi Mwake, na Yeye akafanya kipindi kirefu cha wakati usiopimika katika miaka ya nuru zaidi ya hapo, na hapo akiangalia chini kuliona.

30 Ndipo huyu Mrusi alisema kwamba alikuwa yapata maili mia moja hamsini, mia mbili, juu hewani, na akasema kwamba hakumwona Mungu wala Malaika. Binadamu anaweza kuwa

rahisi jinsi gani? Na kisha kuwazia bilioni zote na trilioni za miaka; na miaka hamsini tu kutoka hapa, alifanya nini, kupasua kuingia katika Umilele.

31 Wanasema kwamba huyu mwanaanga alipaa tu juu, alikuwa juu kwa saa nyingi mno, akaenda mara nyingi, mara kumi na saba kuuzunguka ulimwengu, au chochote kilichokuwa, walisema hata haikuninii...haikuwa sekunde moja katika maisha yake. Alikuwa akisafiri na wakati. Kwa hiyo, unaona, unapenya kuingia katika Umilele. Huo ndio ukuu wa Mungu.

32 Akili zetu haziwezi kuelewa jinsi Yeye alivyo mkuu. Na hata hivyo wakati Yeye anapokuwa tayari kujifunua Mwenyewe, huifanya rahisi sana, huchukua vitu rahisi kufanya hivyo, urahisi wake.

33 Daudi, aliyeonekana kuwa ninii—ninii...kati ya wana wote saba wa Yese, yeye alikuwa ndiye wa mwisho kuletwa mbele ya nabii. Mbona, hata jamaa zake wenyewe wangeweza kucheka, wasingeweza kumwazia maskini Daudi aliyeonekana dhaifu, mwenye mabega yaliyoinama, mtu aliyeonekana dhaifu kuwa mtu ambaye ndiye angeweza kuwa mfalme wa Israeli. Huenda hakuonekana kama mfalme kwa wale watu, bali bila shaka alionekana kama mfalme kwa Mungu, maana wao... Alimpaka mafuta kuwa mfalme, kwa vyovyote vile. Mnaona, Yeye alimchukua aliye mshamba katika familia ya Daudi, au familia ya Yese, ku—kufanya wafalme. Kitu ambacho ulimwengu ulikuwa umekataa, ninii...alikuwa amegeuza, alimtuma huko nyuma kuwachunga kondoo. Alimleta nanii wake—alimleta mwanawe wa kwanza, mtu mkubwa mwenye nguvu aliyeonekana adhimu, labda angeweza kusimama wima na kuonekana kama mfalme wa Israeli, na huyo ndiye waliyefikiria angeonekana wa kupendeza akiwa na taji kichwani mwake, huyo ndiye angeweza kuongoza...kuvaa mavazi ya ki—kifalme na angeweza kuibeba fimbo, na chochote kile kinachofaa kufanyiwa mfalme. A—alionekana wa kupendeza machoni pa watu.

34 Bali nabii, akiwa na mafuta ya kupaka mkononi mwake, alisema, "Huna mwingine?" Ndipo akawaleta, mmoja mmoja, mpaka hatimaye akasema, "Huna mwingine?"

35 Akasema, "Ninaye mmoja, lakini labda hawezi kuwa chochote. Ni maskini jamaa ambaye kwa namna fulani amekauka, yuko kule nje akichunga kondoo."

36 Akasema, "Nenda kamlete." Na punde tu macho ya nabii aliyetiwa mafuta yalipomwona, alimimina mafuta juu ya kichwa—kichwa chake, na kukimbia ili kumlaki. Kasema, "Huyu ndiye ambaye Mungu amemchagua." Mnaona? Mnaona, si mapambo kila mara, ya ulimwenguni. Ni chaguo la Mungu.

37 Na kwa neema Yeye alituchagua, kwa hiyo tuna shukrani kwa hilo asubuhi ya leo. Na haihitaji hayo mambo makuu ya

mapambo ya ulimwenguni. Aliye wa chini kuliko wote anaweza kuwa mtumishi wa Kristo, humchukua mtu aliye tayari.

38 Mungu alimtia upako, unaona, huchukua vitu duni. Sasa, ni kwa nini Yeye akachukua Bethlehemu mdogo? Ilionekana kana kwamba kungekuwa na mahali mashuhuri zaidi ambapo Mfalme, Mfalme mkuu wa wafalme angeweza kuzaliwa.

39 Kwa kawaida tunapoandaa sherehe hapa duniani, tunajaribu kuiweka katika kitu cha juu kuliko vyote, kinachometameta tuwezacho kuwazia, tunaipeleka katika sehemu kubwa kuliko zote na kutumia pesa nyingi, na vitu vilivyonakshiwa kuliko vyote. Hivyo ndivyo tunavyofanya.

40 Lakini Mungu hafanyi namna hiyo. Yeye huchukua kitu duni, kusudi aweze kujionyesha Mwenyewe kuwa ni mwenyezi, kwamba Yeye anaweza...Kama angalichukua kuhani mkuu au mtu aliyefunzwa sawasawa, katika siku alizokuwa akiwaita mitume, iwapo angalichukua hao badala ya mvua samaki asiye na elimu, wala maarifa ambaye asingeweza hata kuandika jina lake mwenyewe, wangalisema, "Loo, hiyo, unaona, elimu yako inakufaidi." Lakini Mungu alimchukua mtu ambaye hakuweza hata kuandika jina lake, kwamba Yeye aliweza kuchukua kitu ambacho angeweza kushika mkononi Mwake, kitu ambacho Yeye angeweza kufanya kitu fulani kutokana nacho, kuonyesha kwamba Yeye ni Mungu. Tunafikia mahali ambapo tunatambua kwamba sisi si kitu, ndipo tunaingia mikononi mwa Mungu, na Yeye anaweza kukufinyanga na kukufanya jinsi anavyokutaka uwe. Lakini mradi tunajisikia kwamba sisi ni muhimu, basi hutafika popote. Hata huwezi kuingia mikononi mwa Mungu mpaka tutambue kwamba sisi si muhimu.

41 Mmoja wa wasichana wangu wadogo alikuwa akiuliza hivi majuzi kuhusu kuwa muhimu. Nikasema...Vema, nikizungumza kuhusu mtu fulani muhimu. Vema, alikuwa ni Rais ambaye alikuwa ndiyo kwanza auawe, na mioyo yetu ilihuzunika juu yake. Nami nikasema, "Vema, huyo alikuwa ni mtu muhimu." Magazeti yalilitangaza, na televisheni kulionyesha, iligharimu serikali mabilioni na mabilioni ya dola kutangaza hilo. Ambalo, hilo ni sawa, hiyo ni kazi yao. Bali nikasema...Maskini huyu mhubiri wa Kipentekoste huko juu Carolina, ambaye mtu aliingia, mlevi akiwa na bunduki ya marisau, akamwita mke wake na akampiga risasi mtu huyo moja kwa moja kutoka mimbarani, kisha akampiga risasi mke wake, na kujipiga risasi mwenyewe, makala ndogo nyuma ya gazeti yapata ukubwa *huo*. Hebu nikwambie, ndugu, haijalishi sisi ni kina nani, "Ukitaka kujua jinsi ulivyo muhimu," nilimwambia maskini msichana wangu, "chomeka kidole chako katika ndoo ya maji halafu ukitoe, kisha ujaribu kutafuta shimo hilo." Sisi si kitu. Kuna Mmoja tu aliye muhimu, huyo ni Mungu. Lazima tukumbuke, Yeye Ndiye.

42 Ilionekana kana kwamba kama wangalitaka ku… wanadamu walikuwa wakiandaa mahali kwa ajili ya Mfalme kuzaliwa, kulikuwa na sehemu mashuhuri zaidi za kidini na sehemu za kihistoria kwa ajili ya Mfalme badala ya Bethlehemu huu mdogo. Mahali, kwa mfano, kama Shilo. Shilo palikuwa ndipo sanduku la agano liliwekwa kwa mara ya kwanza, tunajua, tunapopitia ambapo…tunapovuka Yordani kuja ng'ambo hii katika Palestina, na ambapo sanduku la agano liliwekwa kwa ajili ya mahali pake pa kwanza pa kuabudia. Ama Gilgali; Sayuni, Sayuni mahali mashuhuri; Gilgali, pia.

43 Ama mji mkuu wa kifahari, Yerusalemu, mahali ambapo wakuu wa mashirika yote walikusanyika, makao yao makuu, ilionekana kana kwamba wangeandaa mahali huko Yerusalemu kwa Mfalme mashuhuri kuzaliwa, kama walitaka mahali, mahali pa kihistoria au mahali maalum penye umaarufu. Hapo ndipo palipokuwa na makao makuu ya kidini, ya dini yao ambayo Mfalme alijia. Alikuja kuwakilisha dini yao. Na Yeye… basi wakati Yeye alipokuja, badala ya wao kumwandalia mahali huko Yerusalemu ama moja ya sehemu hizo mashuhuri za kihistoria, Yeye alizaliwa Bethlehemu, mji ulio mdogo kuliko yote. "Je! hu mdogo kuliko wote katika majumbe wa Yuda? Bali kutoka kwako atakuja M—mtawala atakayewatawala watu Wangu." Nao huu Yerusalemu mkuu wenye fahari na miji mingine yote ilikataliwa.

44 Ama labda wangeweza kuchukua baadhi ya mahali pa kimbilio, mahali mashuhuri kama Hebroni, Kadeshi, au Ramoth-gileadi, moja ya hiyo miji mashuhuri ya kimbilio, kwa sababu Yeye alikuwa awe ni Kimbilio letu. Kama tungejaribu kulitunga katika akili zetu wenyewe, huenda tungechukua, tuseme, "Vema, sasa, ikiwa Mfalme huyu mkuu anakuja, ambaye atakuwa Kimbilio letu, Yeye anafaa kuzaliwa katika moja ya sehemu mashuhuri za kumbukumbu za kimbilio, kama Ramoth-Gileadi, ama Kadeshi, au moja ya sehemu hizo." Tungejaribu kulitunga namna hiyo akilini mwetu.

45 Lakini, mnaona, Mungu anazo njia zingine za kufanya mambo. Anajua jinsi ya kufanya mambo ipasavyo. Na sasa kwa nia ya Mungu na msaada wa Mungu, tutajaribu kusema ni kwa nini hili lilitendeka, kwa kuwa mambo yote hufanya kazi sawa hasa katika mpango mkuu wa Mungu. Nami ninawatakeni enyi watu hapa Phoenix, na karibu, ku—ku—kujaribu kupata Hili. Kwamba mkumbuke, kwamba Mungu anajua yale afanyayo. Mnaona? Naye huchukua vyombo duni kuyafanya navyo. Kwa sababu, kama akifanya jambo kwa kitu fulani kikubwa maarufu, basi…Mungu kamwe hafanyi mambo namna hiyo, kamwe hakufanya hivyo katika historia yote ya Biblia. Mungu kamwe hakuwahi kutumia, si katika wakati wowote, kuchukua kundi lolote la watu kufanyia chochote. Mungu humchukua mtu binafsi. Wewe ndiwe, wewe, mtu mmoja. Na Mungu kamwe

habadilishi mpango Wake. Kwa sababu, mpango Wake wa kwanza, Yeye hana budi kudumu na mpango huo daima.

46 Katika siku za Nuhu, alikuwa na mtu mmoja, Nuhu. Siku ambazo aliwatoa Israeli, Yeye alikuwa na mtu mmoja, huyo alikuwa ni Musa. Tunajua Dathani na wengi wengine walijaribu kuwazia, vema, wao "walikuwa na mamlaka yale yale" na kadhalika. Mnajua kilichowafanyikia. Siku za kuja kwa Bwana, siku za Yohana Mbatizaji, na wengine mbalimbali, Yeye ana mtu mmoja ambaye Yeye hutumia. Na Yeye anahusika nasi leo kama mtu binafsi, si kama kikundi. Mtu mmoja! Itakuwa ni juu yangu na wewe, jinsi tunavyosimama mbele za Mungu. Kwa sababu, anahusika na mimi na wewe kama watu binafsi, si kama kundi tulilomo, wala si kama dhehebu la kanisa tunaloshiriki, bali kama mimi na wewe kama watu binafsi.

47 Sasa, Yoshua, katika kuigawa nchi, alimpa Yuda mahali hapa padogo. Wengi wenu, ni—ninazo baadhi ya mahali palipoandikwa ambapo huo hukalia, bali sote tunafahamu jambo hilo, mahali ulipo kwenye kona. Na palikuwa tu ni mahali padogo ambapo waliwapa, Yoshua, katika kuigawa nchi, aliwapa hapo kabila la Yuda.

48 Ndipo sasa wakati Israeli walipovuka mto Yordani, sasa jaribuni kulishika hili, wakati Israeli walipovuka kuingia kwenye nchi, nchi ya ahadi, kulikuwako na mwanamke Mtaifa ambaye tunamjua kama Rahabu kahaba. Na yeye aliomba rehema, na akapata rehema, alipata rehema mradi tu alikaa chini ya ukanda mwekundu. Na hiyo ndiyo njia pekee angaliweza kupata rehema. Ilikuwa ni alama, ishara aliyopewa.

49 Tunayo Ishara leo, pia, na tuko salama mradi tunakaa chini ya ukanda wetu mwekundu, Damu ya Yesu Kristo. Kama mtu binafsi, si kundi, mtu binafsi, kila mmoja lazima tukae chini ya huo ukanda mwekundu wa Damu ya Yesu Kristo.

50 Halafu basi huyu Rahabu, baada ya kuokolewa, aliwaingiza watu wake wote ndani, kila kitu kilichokuwa chini ya ukanda ulikuwa—uliokolewa. Kama tu vile wakati Mungu huko Misri, wakati wote waliokuwa chini ya damu waliokolewa. Wote waliokuwa chini ya ukanda mwekundu waliokolewa. Wote chini ya Damu ya Yesu wameokolewa, wote wasio chini Yake wamepotea na wako tayari kuangamizwa. Pia tunaona sasa, katika kufanya hili. . . Ndipo tunaelewa kwa historia kwamba alichumbiana na jenerali fulani, sijui jina lake hivi sasa, katika jeshi la Israeli. Na hatimaye akaolewa na mwanamume huyu. Nao wakakaa hapa katika, karibu na mahali hapa padogo, na mwanawe, Salmoni, ndiye aliyeanzisha Bethlehemu. Mnaona, Mmataifa ameunganishwa na hilo kwa kuanzia, Mmataifa, Rahabu kahaba.

51 Sasa, tunaona kwamba Salmoni alianzisha mji huu mdogo wa Bethlehemu. Naye akamzaa Boazi. Naye Boazi alikuwa ndiye

aliyemwoa Ruthu, Mmataifa mwingine. Nasi tunaufuata ukoo huu sasa. Ruthu, alipata, alikuwa Mmoabu, naye akaolewa na Boazi, na akaja katika mji huu mdogo katika msimu wa shayiri. Loo, kama tungalikuwa na wakati asubuhi ya leo, mpaka, katika hilo, ningedaiwa na mke wangu magauni sita, baadaye. Lakini jinsi ya kulikalia somo hilo!

52 Naomi, akiwakilisha kanisa la kiothodoksi, aliondoka kwa sababu ya njaa, alienda katika nchi ya Moabu; kama vile kutawanyika kwa Israeli, kote miongoni mwa mataifa. Ndipo basi aliporudi, alirudi pamoja na Ruthu, Mmoabu, naye alirudi tu katika msimu wa shayiri, mavuno ya kwanza ya shayiri. Hiyo ni kwamba Kanisa la Mataifa linamjia Mungu tu katika msimu wa shayiri tena. Ni picha ya kupendeza jinsi gani hapo. Ndiposa yeye na Boazi wakishaoana, na mwana wao maarufu, Obedi, alishikwa mimba pale, na pia kuzaliwa. Halafu basi mwanawe, mwana maarufu, Yese, alitokana na Obedi. Hapo pia akamzaa Daudi, mwanawe, mfalme Daudi akatokea.

53 Angalia hili likija sasa. Kutoka kwa Rahabu kahaba, mwanawe, akiuanzisha. Kutoka kwa huyo akaja—kutoka kwa huyo akaja Boazi, aliyemwingiza Mmataifa mwingine. Ndipo basi kutoka kwa Boazi akaja Yese. Na hapa Yese, kwa Yese akazaliwa Daudi. Naye Daudi, papa hapa kwenye Bethlehemu uu huu mdogo, alipakwa mafuta na nabii wa Mungu, kuwa mfalme wa Israeli. Mambo haya yote ya kiroho yaliyofichwa kutoka kwa macho ya ulimwengu, yalikuwa yakitendeka hapa katika mji huu mdogo wa Bethlehemu. Mnaona, hivyo ndivyo Mungu afanyavyo.

54 Sasa, ninatumaini ya kwamba Roho Mtakatifu atakuwa hapa sasa kuwapa ufahamu mzuri, kwamba Mungu hafanyi kazi katika mambo haya makubwa. Ni kwa Roho. "Si kwa uweza, si kwa nguvu, bali kwa Roho Yangu," asema Bwana. Mnaona? Mungu akifanya kazi katika Roho miongoni mwa watu. Mnaona, misingi hii mashuhuri, Yeye angeweza tu kuja katika mji huu. Hapo ndipo mahali pekee angaliweza kuzaliwa. Mungu akifuata mkondo wake ule ule. Mungu daima hufanya hivyo. Mungu hufuata m—mkondo wa Neno Lake. Hawezi kurudi nyuma kuliacha Neno Lake, kwa vyovyote, na halafu abaki Mungu. Hana budi kudumu na Neno. Hawezi kuacha Hilo. Leo hii, mapokeo yetu na kadhalika hutuondoa kwenye Neno. Tuna kanuni za imani na kadhalika tunazoingiza katika Neno, ambazo huchafua kitu hicho chote. Lakini Mungu hawezi kuacha mkondo wa Neno Lake. Neno Lake ni kweli, daima, kwa sababu Yeye ni Neno. Mungu na Neno Lake ni sawa.

55 Sasa, tunaona hapa jinsi ambavyo Bethlehemu huu mdogo, hata hivyo haukutambulikana, mahali padogo pasipotambulikana sana kwa ulimwengu wa nje, mji tu mdogo kuliko yote, hakuna mtu aliuzingatia. Bali hata hivyo Mungu alikuwa nalo katika kusudi Lake kwamba hapo. . .hapo ndipo

mambo haya yote yangetukia. Sasa, nia ya kiroho ingeshika hilo, kwa sababu nabii alisema hapa, unaona, nabii alisema, "Ewe Bethlehemu ya Yuda, hu mdogo zaidi katika majumbe yote? Bali kutoka kwako atakuja Mtawala ambaye atawatawala watu Wangu Israeli." Nabii, nia ya nabii iliipata.

56 Waangalie hao wa kiroho, Roho Mtakatifu leo hii akiyaongoza mambo hayo. Haileti tofauti yoyote yale ulimwengu usemayo katika mapambo yake yote. Mwangalie Roho Mtakatifu katika Neno, hapo ndipo ilipokuja.

57 Vipi kuhusu wakati Ayubu alipokufa na alitaja bayana mahali pake pa kuzikwa? Baadaye akaja Ibrahimu, Ibrahimu akanunua kipande cha uwanja kumzika mke wake, Sara. Naye Ibrahimu, wakati alipokufa, alitaka kuzikwa pamoja na Sara. Ibrahimu akamzaa Isaka. Isaka, wakati alipokufa, alitaka kuzikwa pamoja na Ibrahimu. Isaka alimzaa Yakobo. Yakobo akafa, huko chini Misri, lakini alimfanya Yusufu (mwana wake nabii) kuapa kwake, huku ameweka mkono wake kwenye nyonga yake legevu, kwamba asingalimzika huko chini Misri. Kwa nini? Kasema, "Nipeleke huko katika nchi na akazikwe huko." Naye Yusufu, wakati alipokufa huko chini Misri, alitaja kuhusu kutoka, na Israeli kuondoka kulingana na unabii, bali alisema, "Ibebe mifupa yangu kutoka katika nchi hii." Kwa nini? Walijua malimbuko ya ufufuo yalikuwa yanakuja kutoka katika nchi hiyo, kwa sababu Ayubu alisema, "Ninajua Mkombozi wangu yu hai, na katika siku za mwisho Yeye atasimama juu ya nchi; na ijapokuwa mabuu wa ngozi wauharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu."

58 Walijua kuwa malimbuko ya ufufuo yalikuwa yanakuja kutoka kwenye nchi ya ahadi, si Misri. Walikuwa ni wa kiroho, walikuwa manabii. Na wakati Yesu alipokufa, kwenye—kwenye Ijumaa Kuu, na akafufuka asubuhi ya Pasaka, Jumapili iliyofuata asubuhi, Biblia ilisema ya kwamba, "Wengi wa watakatifu waliolala katika mavumbi ya nchi, walifufuka na kutoka makaburini, wakaingia mjini, wakapaa kwenda Utukufuni pamoja na Yeye." Kwa nini? Ilikuwa ni hao manabii waliojua hasa mahali pa kuzikwa, kwenye mahali na kwenye wakati. Ilifichwa macho ya wenye hekima. Bali wao walijua kile—kile, waliangalia upande wa Roho. Ma—malimbuko ya ufufuo yalikuwa yaje kutoka Palestina, si kutoka Misri.

59 Ndivyo ilivyo leo hii, marafiki. Watu wengi sana hushikilia mambo ya ulimwengu, ama mfumo fulani mashuhuri au kitu fulani. Nizike ndani ya Yesu, kwa kuwa wale walio ndani ya Kristo Mungu atawaleta pamoja na Yeye katika huo ufufuo. Na mimi sijali kile ulimwengu utakacho kusema, jinsi wanavyojaribu kupamba vitu. Ni katika Kristo, wale walio ndani ya Kristo hao Mungu atawaleta pamoja na Yeye. Nia ya kiroho huyashika hayo mambo ya kiroho.

60 Hapa nabii alisema, “Bethlehemu mdogo, hivi wewe siye mdogo kuliko wote miongoni mwa majumbe wote wa Yuda? Lakini kutoka kwako atakuja huyu Mtawala,” si kutoka kwenye makao makuu yaliyojiendeleza, si kutoka katika uwanja wa kanisa fulani la kihistoria au kitu fulani, ambapo Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Pentekoste, au chochote kile kilipoanza. “Bali kutoka kwa mdogo zaidi kati ya hawa, kutoka mahali padogo pasipo na maana nitapaleta mahali hapa, Mtawala Wangu wa watu.”

61 Lakini leo hii tunataka kusema, “Baba zetu walifanya *hili*, na baba zetu walifanya *lile*.” Mnaona, Mungu hupuuza kila sehemu ya hayo. Mungu hufanya atakayo. Angalia mkondo wa Roho, angalia jinsi ambavyo Ma—Maandiko yanavyosema. Hawakujua hayo. Bali, mnaona, Maandiko ndiyo yaliyo sahihi. Daima, Mungu yuko sahihi.

62 Daudi alipakwa mafuta na huyu nabii mashuhuri, kuwa mfalme. Hapana shaka kwamba Samweli, huyu nabii mashuhuri, aliyajua mambo haya kimbele. Na ilikuwa hapo ambapo mbegu yake kuu ya kiroho iliyoahidiwa . . . kwa kuwa Mungu aliapa kwa kiapo, kwamba atamwinua Kristo aketi juu ya kiti cha enzi cha Daudi. Basi ni wapi pengine ambapo Kristo angezaliwa? Huyu hapa baba Yake amezaliwa, babu Yake, babu wa baba Yake, babu wa baba wa baba wa baba wa baba wa baba huko nyuma. Mnaona, watu Wake katika ukoo wa Mataifa waliingizwa. Na sasa Biblia ilisema kwamba, “Mataifa watatumainia katika Jina Lake.”

63 Mnaona, yote hayana budi kuletwa ndani kusudi mweze kuyaona. Tungependa kukaa hapo kwa muda na kukaa katika hilo, na kuwaonyesha ni kwa nini Mataifa, bali nina hakika nia ya kiroho itashika hili mara moja sasa; kwa sababu, kwa kuwa ni kina mama, na si baba. Sasa, maana i—ilikuwa ni mwanamke, Bibi-arusi. Mataifa wataumbika, Bibi-arusi, ataumbwa kutokana na Mataifa. Mmataifa, “Yeye atawatoa watu kutoka kwa Mataifa kwa ajili ya Jina Lake.” Hilo ni Jina Lake. Alimchukua mke, unaona, kutoka kwa Mataifa. Na hivyo ndivyo ilibidi iwe, mwanamke aliingia, kanisa, na yeye . . . walikuwa ni Mataifa, nyanya zao huko nyuma katika mkondo wa mbegu.

64 Sasa, kama tu vile Isaka alivyokuwa katika mkondo wa mbegu vinginevyo. Sasa angalia hili, tunaona basi kwamba Daudi alikuwa na ahadi hii ya mwana. Sasa, tunaona jinsi ambavyo hilo linaambatana tena na Israeli. Wakati Israeli . . . Ama Ibrahimu aliahidiwa kwamba mzao wake, kile kingekuwa, kwamba kutokana na mzao wake atakuja huyu Mwokozi mkuu, naye atakuwa baba wa mataifa. Mzao wake wa kimwili, bila shaka, alikuwa ni Isaka, naye alishindwa. Lakini Mzao wake wa kiroho, kwa imani aliyokuwa nayo, alikuja Kristo, ambaye aliingiza mataifa yote.

65 Vema, sasa jambo lile lile limefananishwa hapa tena. Mzao wa Daudi wa kimwili alikuwa ni Sulemani, naye alirudi nyuma tu kama yule mzao mwingine wa Ibrahimu alivyofanya. Alirudi nyuma. Ndivyo na Sulemani alivyorudi nyuma. Alichukua wanawake wengi sana na, muda si muda mwajua, walitoa roho yake kwa Mungu. Na jinsi alivyoenenda na kurudi nyuma, alikufa namna hiyo, akarudi nyuma. Israeli walikufa kwa njia iyo hiyo, walirudi nyuma.

66 Lakini tunaona kwamba Mzao huu wa kiroho, aliyeahidiwa kwa mzao wa kimwili kama ukoo wa watu unaokuja kupitia Ibrahimu, bali kama ufalme ulivyokuja kupitia ahadi ya kiroho ya Daudi. Naye Daudi alizaliwa Bethlehemu. Pia alitiwa mafuta Bethlehemu. Ndipo tunaona basi ya kwamba wakati Mzao wake halisi wa Kifalme, Mrithi wa kiti chake cha enzi alipozaliwa, katika mji uu huu, Bethlehemu mdogo. "Wewe u mdogo katika majumbe wote wa Yuda, bali kutoka kwako atakuja Mtawala atakayewatawala watu Wangu."

67 Katika mji huu mdogo, zizi dogo, zizi la mjini huko chini ubavuni mwa genge, kulikuwako na pango katika genge, na kutoka hapo akaja kupitia malango yake madogo, Mfalme wa Amani, aliyezaliwa kwenye zizi, katika ki—kisanduku kidogo cha—cha nyasi kavu kilichowekwa mahali fulani, samadi imelundikwa katika vibanda, na kadhalika, lakini kutoka hapo akaja yule Mfalme mkuu, Mzao wa mwanamke, kutoka hapo akaja Mwokozi wa ulimwengu, kutoka hapo akaja Yehova Mwenyewe, katika umbo la mwanadamu, alikuja kutoka kwenye maskini zizi hilo duni huko Bethlehemu. Si katika ikulu ya mfalme fulani, akizaliwa katika jamaa ya kifalme; lakini hapo Yeye alikuja kutoka mahali hapo panyenyekevu, kwa lundo la samadi huko chini, na alifunikwa nguo za kitoto. Kama mafundisho yaliyotokea zamani yasemavyo, zilitolewa kwenye nira ya maksai ambapo walikuwa wakilima nayo.

68 Watu maskini! Yusufu na Mariamu, wote wawili maskini hohehahe, na hapa walikuwa katika zizi hili dogo. Jinsi Mungu anavyojinyenyekeza Mwenyewe! Na halafu sisi tunajaribu kujifanya kitu fulani kikuu. Hamwezi kuona jinsi Mungu hujinyenyekeza Mwenyewe na kuchukua kitu kisicho, kusudi Yeye aweze kutimiza ahadi Zake kuu. Jinsi ambavyo mtoto Yehova amelala katika hori, amefungwa ngu—nguo iliyotolewa kutoka nyuma ya nira, shingo ya nira ambapo maksai alikuwa. Na kumfunga Mfalme wa Amani katika hiyo! Jamani! Sisi ni kina nani basi? Tunastahili nini? Kama Mungu anaweza kujinyenyekeza Mwenyewe namna hiyo, si inatupasa kuweza kujinyenyekeza wenyewe kuwa mtumishi Wake, kama Yeye alifanya mambo namna hiyo? Hivi hatuwezi kusahau hadhi zetu kubwa na mambo ya ulimwengu, na tupite kutoka kwenye hayo, na kujinyenyekeza wenyewe mbele Zake Krismasi hii? Na kuwa ninii . . . Kumwonyesha Yeye shukrani zetu za kuzaliwa huko na

unyenyekevu huo, kwa kujinyenyekeza wenyewe na kulipokea Neno Lake. Haijalishi yale mapokeo yasemayo, ni Neno Lake ndilo linajalisha. Hilo ndilo atakalochukua, Neno Lake, na Hilo pekee.

69 Sasa tunaona, zizi hili dogo, ni hapo ndipo noeli ya kwanza ilipopata kuimbwa duniani, nayo iliimbwa na Malaika. Wazia hilo! Noeli ya kwanza, si kuimbwa huko juu na Kayafa, si huko chini kwenye kanisa fulani maridadi mahali mchungaji wa ajabu alipokuwa, bali kwenye zizi huko Bethlehemu, mdogo wa hao wote. Lakini noeli ya kwanza iliimbwa na Viumbe vya Kimalaika katika mji mdogo wa Bethlehemu. Mnaona ninachomaanisha?

70 Haijalishi jinsi ulivyo maskini, jinsi gani huenda wewe—wewe ni mdogo au asiye na maana, Mungu anaweza kukutumia ikiwa tu utamruhusu kufanya hivyo. Mungu anakutaka wewe. Hakutaki uninii. . . si lazima uwe mwanachama wa jumuiya fulani mashuhuri, utaratibu fulani mashuhuri, udugu fulani mashuhuri, ama chochote kile, hiyo haimaanishi chochote kwa Mungu. Mungu anakutaka wewe! Na kama wewe ni. . . kama unajihisi kuwa wewe ni mashuhuri, iondoe hisia hiyo kutoka kwako. Inakubidi kuiondoa. Unasema, "Vema, vema, nina Ph.D., LLD." Hiyo inakupeleka tu mbali kiasi hicho kutoka kwa Mungu. Kisahau kitu hicho. Mrudie Mungu. Rudi kwenye unyenyekevu wa Roho, na umpende Mungu na kulichukua Neno Lake.

71 "Tena mkikaa ndani Yangu na Neno Langu ndani yenu, basi ombeni mtakalo, mtapewa." Mungu aliahidi hilo. "Ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka,' wala usitie shaka moyoni mwako, bali uamini kwamba yale uliyosema yatatimia, unaweza kupata uliyosema." "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo naye pia atazifanya. Hata kuu kuliko hizi atafanya, kwa kuwa ninaenda kwa Baba Yangu." Ahadi jinsi gani!

72 Kuna kitu kinachokosekana mahali fulani. Tunachojaribu kufanya ni kuipinda na kuifanya kitu fulani kikubwa huko juu, kuweka ua na mapambo juu yake, na tunaichafua tu kama vile mataifa yameichafua Krismasi. Hiyo ni kweli! Laiti tungaliweza kuondoa mapambo kwenye vitu hivyo, na kurudisha u—unyenyekevu katika moyo wa mwanadamu! Laiti tungaliweza kurudisha unyenyekevu kwa Krismasi wa kile inachopaswa kuwa! Si siku ya biashara, si vimulimuli na Baba Krismasi! Bali kurudi katika kumwabudu Mungu wa uumbaji Yule aliyekuja katika zizi na akazaliwa Mtoto, Mungu aliyefanyika mwili na kukaa katikati yetu! Laiti tungaliweza kurudi kwa hilo, tuyaondokee mapambo na vitu vikubwa. Mungu hata hahusiki navyo hata kidogo.

73 Unasema, "Vema, mimi ni mshiriki wa dhehebu kubwa kuliko yote." Hiyo inakupeleka mbali na Mungu kiasi hicho.

Unasema, "Mimi hufanya *hili*, lile." Hiyo inakupeleka tu mbali kiasi hicho.

74 Inakubidi kujinyenyekeza mpaka uone hilo, mpaka, "Mkikaa ndani Yangu na Maneno Yangu yakae ndani yenu, basi ombeni mtakalo." Kile tunachojaribu kufanya, punde tu Mungu anapotupatia nyunyizo dogo la baraka, tunajaribu kulipindua lote na kuwaingiza wenye vyeo mle ambao wanaenda kufanya majina makubwa mashuhuri na kumshinda yule mwingine. Huyu anaanza *huku* na *kule*, Mungu anaacha kitu hicho chote. Kile tunachohitaji leo hii ni kumiminwa upya kwa Roho Mtakatifu juu ya mioyo iliyo minyenyekevu. Tunahitaji Krismasi halisi, mahali pa kuzaliwa. Laiti ungaliweza kutambua kwamba wewe si kitu ila zizi! Mungu hakuenda Yerusalemu, Shilo, ama Ramoth-Gileadi, Yeye alikuja katika zizi lililochafuliwa. Ukimruhusu Mungu, unakuwa. . .na kutambua ndani yako kwamba wewe si kitu ila zizi linalonuka. Lakini karibisha, ifungue milango yako, wakati sehemu hizi kubwa na vyumba vya wageni vinamkataa, ifungue milango yako ya hori ya moyo wako na kuruhusu Yehova aingie katika hiyo, na uone kinachotendeka, kwa kuwa Yeye ni Neno. Yeye alisema, "Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu." Yeye ni Neno. Mwache aingie ndani yako, na uone kinachotendeka. Ndipo uombe utakacho, na utatendewa.

75 Naam, ilikuwa pale noeli ya kwanza ilipoimbwa na Malaika, miaka mingi iliyopita. Na wakati Yeye . . .

76 [Ndugu mmoja ananena katika lugha nyingine. Mtu fulani anatoa tafsiri. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Na sasa tunajua ya kwamba hapana shaka ujumbe ni muhimu sana, hata Mungu alitaka kusema hivyo, la sivyo Yeye asingalikatiza ujumbe kufanya kitu kama hicho. "Jinyenyekezeni chini ya mikono ya Mungu," ulikuwa ndio ujumbe wake, enyi marafiki.

Sasa, Baba yetu wa Mbinguni, tunajua kwamba Wewe ni hekima yote na hufanya kila kitu sahihi. Tunaomba kwamba Wewe utajalia sasa kwamba huu uweze kuwa u—ujumbe kwa watu, kwamba kwa kweli lazima tujinyenyekeze, sisi sote, na kuja chini ya mkono wa Mungu mwenyezi. Tunajikabidhi Kwako, Baba, kwamba Wewe utatujalia hili. Katika Jina la Yesu, Mwanao. Amina.

77 Sasa, ili kuendelea, nilikuwa nikizungumzia ambapo noeli ya kwanza iliimbwa, iliimbwa na Malaika huko Bethlehemu mdogo. Huko ndiko watu hawa wote mashuhuri walikozaliwa. Huko ndiko ahadi ya Mfalme ilikozaliwa. Mfalme aliyeahidiwa alikuja kwenye huo. Sasa, neno. . .kufanya upesi sasa, kusudi nisiwaweke kwa muda mrefu kupita kiasi. A—ahadi, neno lilikuwa hili, neno "Bethlehemu." Hebu tulichambue. Niliruka mambo machache niliyoandika hapa ili kuokoa wakati.

Sasa, Bethlehemu. Neno *B-e-t-h* linamaanisha “nyumba.” *E-l* linamaanisha “Mungu,” katika Kiebrania. *E-l-h-e-m* ni “Mkate.” *Bethlehemu*, “nyumba ya Mkate wa Mungu.” Hilo ndilo neno hilo linalomaanisha.

78 Maneno, majina, yana maana. Watu wengi hawaamini hilo, lakini hilo ni kweli. Ikiwa majina hayana maana fulani, ni kwa nini ilibidi jina la Abramu kubadilishwa kuwa Ibrahimu? Ni kwa nini ilibidi Sarai kubadilishwa kuwa Sara? Ni kwa nini ilibidi Sauli kubadilishwa kuwa Paulo? Ni kwa nini ilibidi Simoni kubadilishwa kuwa Petro? Unaona, haya yote yana maana, kila kitu kina maana.

79 Nalo jina *Bethlehemu* linamaanisha “nyumba ya Mkate wa Mungu.” Sasa, jinsi hiyo inavyomfaa Yesu, Mkate wa Uzima wa Milele. Kristo ndiye Mkate wa Uzima. Sote tunaamini hilo, sivyo? Jinsi Bethlehemu inavyofaa hapo, kituo cha mkate cha ulimwengu, kilikuwa kituo cha mkate wa Uzima wa Milele. Hiyo ndiyo sababu ilibidi Mfalme azaliwe huko. Yeye alisema, katika Yohana Mtakatifu 6:35, “Mimi ndimi Mkate wa Uzima uliotoka kwa Mungu Mbinguni. Baba zenu walikula mana nyikani, na wote wamekufa. Lakini Mkate huu, mtu akila Mkate huu, ataishi milele.” Basi, Yesu ni Mkate wa Uzima, kwa hiyo Mkate wa Uzima ilibidi uje Bethlehemu. Yeye ndiye Mkate wetu wa Uzima kwa ajili ya safari, kama vile Israeli. Mungu aliwapa Israeli mkate kutoka angani, kwa ajili ya safari yao, waliposafiri kutoka mahali walipotoka Misri kwenda nchi ya ahadi. Mkate, kila usiku, ulishuka kutoka angani. Pia Mungu alitupa Mkate wa Uzima kwa ajili ya safari yetu, ulioshuka Bethlehemu, nyumba ya Mungu ya Mkate. Unaona jinsi ilivyobidi iwe? Sharti iwe ni mahali jina hilo linapoitwa, *Bethlehemu*, “nyumba ya Mkate wa Mungu.” Basi angewezaje kuzaliwa Yerusalemu? Angewezaje kuzaliwa Ramoth-Gileadi? Unaona, Yeye alikuja mahali Jina Lake lilipokuwa, “nyumba ya Mkate wa Mungu.”

80 Loo, tazama, Israeli ilipokea mkate mpya safi kila usiku, ukishuka kutoka Mbinguni, kwa ajili ya safari yao. Kristo ndiye Uzima wetu, Mkate wa Uzima, na kila siku tunapokea burudiko kutoka kwa Kristo, kutoka Mbinguni, Roho Mtakatifu akishuka juu ya mwaminio kila siku. Mpya!

81 Tukio la jana, wengi wetu wanaishi kwa tukio la jana. Hatupaswi kufanya hivyo. Ni tukio la leo hii! Hiyo ndiyo shida ya madhehebu yetu, wanaishi juu ya tukio la John Wesley, juu ya tukio la Dwight Moody, Finney, Sanky, Knox, Calvin, wengi wa hao huko nyuma. Wanaishi juu ya tukio hilo. Bali, kumbukeni, mkate ulioshuka, na wakajaribu kuuweka hadi kesho yake, uliharibika, wadudu waliingia ndani yake, ukawa na vifurukuta mikia. Na hiyo ndiyo shida leo hii, mabirika yaliyochafuka, wakiishi kwa mkate wa wakati uliopita ambao umeharibika.

82 Lazima tuwe na kitu kipya kutoka kwa Kristo, Neno Lake leo hii kwa ajili ya wakati huu. Mnaona? Yeye ndiye burudani yetu, Mkate wetu ambao hushuka kila siku kutoka Mbinguni juu ya mwaminio. Yeye ndiye Bethlehemu yetu, Nyumba ya Mungu ya Mkate wa Uzima wa Milele. Kristo alizaliwa Bethlehemu, na akafanyika Nyumba ya Mungu ya Mkate wa Uzima wa Milele. Yeye ndiye Mkate wa Uzima. Yeye ndiye Bethlehemu yetu. Kristo ndiye Bethlehemu yetu. Mkate wa kawaida unaitwa "nguzo ya uhai." Tunaita mkate wa kawaida, kama mkate wetu mwembamba, na vitu tunavyopata, vinaitwa nguzo ya uhai. Yesu ndiye Nguzo ya Uzima wa Mungu, Ngu—Ngu—Nguzo ya Mkate wa Uzima kwa ajili ya Uzima wa Milele. Kama vile nguzo ya uhai inaitwa mkate, Yesu, akiwa ndiye Mkate wa Uzima, ni Nguzo ya Mungu ya Mkate wa Uzima wa Milele kwetu. Mnaona?

83 Hatuwezi kuenda, kitu fulani hakina budi kufa ili tuweze kula. Asubuhi ya leo ukila, unakula kitu kilichokufa. Kitu fulani kisipokufa, basi huwezi kuishi, maana unaishi tu kwa kitu kilichokufa. Ukila nyama, nguruwe alikufa. Ukila nyama ya nguruwe, nguruwe alikufa, bila shaka. Na halafu ukila nyama ya ng'ombe, ng'ombe alikufa. Unasema, "Lakini mimi hula mkate." Basi ngano ilikufa. "Mbona, mimi nilikula mboga za majani." Mboga zilikufa. Unaishi tu kwa kitu kilichokufa, na hiyo ndiyo njia pekee uwezayo kuishi.

84 Basi ikiwa unaweza tu kuishi kwa kawaida, kwa kitu kilichokufa, kitu fulani ilibidi kife ili uweze kuishi kimwili, ni zaidi vipi Kitu fulani hakina budi kufa ili uishi Milele! Kristo alikufa, ili tuweze kuishi Milele. Na Yeye akafanyika Nyumba ya Mkate wa Mungu wa Uzima wa Milele, tunaoshika, mpya, kila majira ya siku, ukishuka kutoka kwa Mungu Mbinguni, katika umbo la Roho Mtakatifu, unalisha nafsi zetu zenye njaa tunapoketi pamoja katika mahali pa Mbinguni. Yeye ndiye Bethlehemu yetu.

85 Basi wana wote wa Mungu wanaoamini kweli wanazaliwa Bethlehemu pamoja na Yeye. Kama ilibidi Kristo afanyike Mkate wa Uzima, kuzaliwa Bethlehemu, ambayo ni Nyumba ya Mkate wa Uzima, basi kila mmoja wa waaminio halisi katika Kristo anazaliwa ndani ya Kristo, wanazaliwa katika Bethlehemu ya Mungu. Amina. Basi, ni kwamba tu, Yesu alizaliwa Bethlehemu, nilizaliwa Bethlehemu, ulizaliwa Bethlehemu. Ulifanyaje hilo? Papa hapa Phoenix, Arizona, asubuhi hii katika Ramada, unaweza kuzaliwa upya katika Bethlehemu ya Mungu, Nyumba ya Mkate wa Milele wa Uzima. Kula Huo na uishi milele!

86 Kwa nini Bethlehemu mdogo? Hiyo ni leo, "Kwa nini kundi la maskini watakatifu wanaojibingirisha? Kwa nini *hiki*, *kile*, au *kinginecho*?" Watu hawajui yote haya yanahusu nini.

87 Bali Roho hufunua Hilo. Neno huonyesha Hilo. Ni madhihirisho ya Neno la Mungu. Tuna Uzima kupitia Kristo,

na Yeye pekee. Mashirika yetu, madhehebu yetu, tofauti zetu, hututenganisha tu na Mungu. Tuna njia moja ya kumfikia Mungu, na hiyo ni kupitia Yesu Kristo. Hakuna njia nyingine tunayoweza kupitia Kwake; hakuna kasisi, hakuna mhubiri, hakuna mfumo, wala chochote kingine; ni Yesu Kristo pekee na Yeye aliyesulubiwa. Yeye ni Mkate wa Mungu wa Uzima, na sisi tunazaliwa ndani Yake. Na kama Yeye ni Mkate wa Mungu wa Uzima, basi Yeye ni Bethlehemu. Na tukizaliwa ndani ya Kristo, basi tumezaliwa na Mungu Bethlehemu, ndani ya Kristo Yesu, tumeketi pamoja katika mahali pa Mbinguni, tukimla Yeye. Tukimla Yeye! Yeye ni nani? Yeye ni Neno. "Hapo mwanzo alikuweko Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." Na wakati tunapoweza kuketi tukiwa na nia moja, Neno la Mungu, na kula Hilo, tuko katika Bethlehemu ya Mungu ya kiroho, tukila Mkate wa kiroho wa Mungu, huku nafsi zetu zikiitikia kila Neno alilonena, kwa "Amina!" Tunafurahia Chakula hiki cha Kimbinguni cha Malaika.

88 Wakati Hilo linaposema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Kanuni ya imani ama dhehebu linasema, "Loo, Hilo sivyo lilivyo." Bali mtu halisi ambaye amezaliwa Bethlehemu, anasema, "Amina!"

89 "Kazi nizifanyazo Mimi nyinyi nanyi mtazifanya." Dhehebu linasema, "Ni lundo la mhemuko wa kujichochea." Bali mkaaji halisi wa Bethlehemu anasema, "Amina," kwa sababu ametosheka, Hicho ni Chakula cha malaika.

90 "Mkikaa ndani Yangu na Maneno Yangu ndani yenu, ombeni mtakalo, nanyi mtatendewa." Amina.

91 Loo, wenye vyeo na wenye hekima hawataliona. Tunashikilia sana desturi zetu za wazee, sana hata inatubidi kubeba kadi na kila kitu kingine kuingia kwenye mimbara fulani. Hizo sizo. Unaweza kuingia kwenye mimbara ya Mungu kwa kujinyenyekeza. Njoo katika Nyumba ya Mkate wa Uzima, Yesu Kristo, na uishi milele katika Uwepo Wake, na kuinuliwa juu mahali pa Mbingu katika Kristo Yesu, ukila Neno. Hilo ndilo Bethlehemu ya Mungu.

92 Ni wangapi kati yetu walioko ndani ya Hilo asubuhi ya leo? Ni wangapi walio tayari kusahau mapokeo yenu, ni wangapi walio tayari kusahau kanuni yenu ya imani ambayo haikubaliani na Neno? Ni kwa nini hatuna uamsho? Ni kwa nini hatuna mambo haya yakiendelea? Pentekoste ina shida gani? Ilijiundia dhehebu. Jambo ndilo hilo. Huwezi kuifanya Pentekoste kuwa dhehebu. Unaweza kuunda dhehebu. Bali pentekoste ni baraka, ni Nguvu za Mungu. Na kama ni pentekoste halisi, kamwe haitaruka Neno kwa ajili ya kanuni ya imani. Itachukua Neno. Kweli, kwa sababu imetahiriwa kutoka kwa ulimwengu na mambo ya ulimwengu. Inatulia tu juu ya Neno la Mungu, na kuamini Hilo. Tuko Bethlehemu, wataradhia wa Ufalme

wa Mungu. Tunakula Mkate wa Mungu wa Uzima wa Milele. Alizaliwa, Mungu Mkate, alizaliwa Bethlehemu, kufanyika Mkate wa Uzima wa kiroho, wa Uzima wa Milele, katika nyumba ya Mungu. Loo, jamani! Kuzaliwa Bethlehemu, ndivyo tulivyo, asubuhi ya leo, wakati tunapozaliwa katika Yesu Kristo, kwa kuwa Yeye ndiye Bethlehemu ya Mungu. Yesu ni Nyumba ya Mungu ya Mkate wa Uzima wa Milele.

93 Yeye pia ni Maji yetu kwa ajili ya safari. Sasa, tunajua ya kwamba Yeye ndiye Maji. Kama vile Israeli katika safari yao, ama walipiga mwamba na mkate wao ukashuka kutoka Mbinguni, bali mwamba ulipigwa kusudi waweze kunywa kutoka kwake kwa ajili ya kuyadumisha maisha yao safarini. Mungu alipiga mwamba, ama alimfanya Musa kuupiga, nabii Wake, aliupiga mwamba. Ilikuwa ni kitu gani? Fungua mwamba. Kama . . . Mwamba ulikuwa ni Kristo. Je! mnaamini hilo? Vema. Basi ikiwa nabii alifungua mwamba huo ili uhai uweze kutoka, basi, kama ni Mwamba, leo tunahitaji Roho Mtakatifu ndani ya mtu fulani atakayeupiga Mwamba tena, amina, na kuliruhusu Neno litoke, kwa sababu Yeye ni Neno.

94 Tumepitia kando kwenye kanuni za imani na kunywa maji yaliyotuama kutoka katika mabirika. Tunachohitaji leo ni kufunguliwa kwa Neno liishilo, na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Hawezi kushindwa. Wanaweza kuliita kuwasiliana kiakili, wanaweza kusema lolote watakalo, ama wenye kuamini kuwasiliana na pepo, ama—ama ibilisi, mradi tu Neno hilo linatembea kwa njia huru na kuzalisha kile hasa ambacho Hilo lilisema litafanya, ni Chemichemi katika nyumba ya Daudi tena, kurudi Bethlehemu, ambapo kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, kwa wakaaji Wake wa Bethlehemu. Ishi na Hilo, ishi ndani ya Hilo, ni Maji ya Uzima safarini kwetu kama Israeli walivyokuwa nayo.

95 Moja ya matukio makuu ya Daudi mashuhuri, kama unataka kusoma kulihusu katika Samueli wa Pili 35:15, kuanzia, tunasoma hapo kwamba Daudi, akizaliwa Bethlehemu, bali hata hivyo akawa mtoro. Loo, ni tamasha ya jinsi gani! Wafilisti walikuwa wamezungukwa na askari wakati huo, nchini, kwa sababu Sauli, mtu mashuhuri aliyeingiza Israeli yote katika dhambi, alikuwa ameanguka kutoka kwa Mungu na kuwa adui wa Mungu, na alikuwa—alikuwa amezungukwa na askari, Wafilisti walikuwa wamezunguka Bethlehemu. Naye Daudi, akijaribu kurudi kwa makao yake mwenyewe, asingeweza kurudi, alikuwa nje nyikani kwa sababu alishakuwa mtoro kwa watu hao, ama, alikuwa amefukuzwa hapo.

96 Ni picha nzuri jinsi gani ya Kristo hiyo iliyo leo hii, mtoro. Ndivyo alivyo. Sasa, unasema, "Hiyo haiwezekani." Vema, kama unaamini Biblia, ndivyo ilivyo. Biblia ilisema, katika Wakati wa Kanisa la Laodikia, kwamba Kristo alikuwa nje ya kanisa, akibisha [Ndugu Branham anagonga mimbarani—

Mh.] akijaribu kurudi ndani ya kanisa Lake mwenyewe. Mtoro ni kitu ambacho kimekanwa, kimekataliwa. Na Neno na Roho Mtakatifu vimekataliwa. Hiyo ni kweli. Huwezi kuingia humo. Kama ukiwahi kumpokea Yeye, inakubidi kutoka humo ili kumpata. Inakubidi kutoka nje ili kumwendea. Yeye hawezi kuingia ndani. Wamekita mizizi sana katika kanuni zao za imani hata ha—hawatakuruhusu kuyahubiri mambo hayo, hawakuruhusu kuamini mambo hayo.

Wanasema, "Je! unaamini kuwa Yeye ni yule yule?"

97 "Loo, kwa njia fulani, Yeye ni yule yule." Sasa, huko si kuishi Bethlehemu. La, la. Huko ni kunywa kwenye birika lililotuama, huko nyuma, mkate wa kale uliooza ambao ulishuka miaka kadhaa iliyopita. "*Fulani-wa-fulani* alisema nini kuhusu Hilo?" Huenda walikuwa sahihi katika siku yao. Hii ni siku nyingine. Hii ni Siku ya Bwana! Huu ni wakati mwingine wa kanisa, si wa Filadelfia. Huu ni wa Laodikia. Ni wa kukataliwa, naye Kristo amekuwa mtoro katika kanisa Lake mwenyewe, amesukumwa nje. Yeye ni mgeni.

98 Anaweza kushuka moja kwa moja na kufanya kazi moja kwa moja miongoni mwa watu, na kufanya mambo yale yale ambayo Yeye alifanya hapa, akisema kwamba Yeye angeyafanya katika siku za mwisho, kutoa ishara zile zile na mambo ambayo Yeye alisema angefanya katika siku za Sodoma. Tunajua yale aliyolifanyia Kanisa pale.

99 Tunamwona Billy Graham, kama ilivyokuwa. Hao wajumbe walishuka kwenda kwenye kanisa la kidhehebu, na kuhubiri mle ndani, na hapo kuwaita watoke, kuwaambia waamini Neno na kutoka Sodoma.

100 Kundi la Ibrahimu halikuwa Sodoma, walikuwa tayari wameitwa wakatoka nje. Mwangalie yule Malaika, kile alichowafanyia kule juu, kwa ajili ya ishara, ambayo waliijua. Na jambo lilo hilo linaweza kufanywa, na watu waseme, "Loo, vema, hatuamini Hilo." Kwa nini? Kwa nini? Kwa sababu kuwa wamemfanya Kristo mtoro kwa shirika lao, ni wageni kabisa na Hilo, Pentekoste na yote pamoja. Sasa, hiyo ni Kweli kabisa. Ninajua hilo linauma. Bali, sikiliza, kama chochote ambacho hakininii. . . Kama—kama ni Kweli, itauma. Na hiyo ni kweli. Halina budi kuwa ni Kweli.

101 Sasa, sasa mwangalie Daudi, wakati alipokuwa huko juu, Daudi aliota kuhusu ushindi wake mkuu. Alikuwa kwenye pango, akiishi huko nyuma, na mbali, yapata maili kumi na tano nje ya mji. Ndipo akajitokeza na kutambua kwamba pale, mji wake wenyewe alioupenda ambapo alikuwa amezaliwa, na mahali alipokuwa amepakwa mafuta kuwa mfalme, na—na kadhalika hapo.

102 Wakaaji wa Israeli, katika siku hizo, walikuwa ni kitu mfano wa ilivyo katika Ujerumani leo hii. Wana miji midogo midogo.

Na halafu wanaishi katika majiji kwa ajili ya usalama, na halafu wanapeleka kondoo wao na mifugo huko nje mashambani na kuwalisha, ndipo wanawarudisha. Ndipo wakati wa jioni, wanawaweka mazizini.

103 Ndipo Daudi, akiangalia chini kwenye mji, alianza kukumbuka matendo makuu ambayo Mungu alikuwa amefanya na yeye, ushindi mkubwa wenye nguvu ambao Mungu alikuwa ameshinda na yeye. Jinsi ambavyo siku moja wakati alipokuwa na kondoo wake huko juu milimani mahali alipokuwa, akilala pale chini kwenye malisho mabichi, na kadhalika, dubu aliingia na kumpata mwana kondoo mmoja na kumnyakua. Ndipo akamfuata, na akamwua huyo dubu. Mungu alimpa ushindi kwa sababu alitumwa na baba yake kuwatunza kondoo hao. Hiyo ilikuwa ninii yake—hiyo ilikuwa ni kazi yake, kuwatunza kondoo!

104 Ee mchungaji, hiyo ni kazi yako! Na wao hula Chakula cha kondoo, sio vitabu vya orodha. Chakula cha kondoo, Neno la Mungu!

105 Mtu mwingine aliingia na kumchukua mmoja, akatoka mbio. Mtu mwingine aliingia na kumnyakua mmoja na kutoroka mbio, alimfuata. Simba aliingia na kumnyakua mmoja, alimfuata. Hakuridhika mpaka alipompata.

106 Hiyo ilimpa ushindi huo mkuu siku moja, wakati alipoona Israeli wote wamekabwa. Mnaona, Israeli ilikuwa ikisikia kanuni zote za imani na kila kitu. Walikuwa na kila kitu, wote walienda kanisani. Wote walikuwa wametahiriwa. Wote walimwendea kasisi na kupata baraka zao kabla hawajaenda vitani. Lakini ilipofikia kwenye shindano la kuamua, la Kiumbe cha Kimbinguni, walikuwa, kila mmoja, waoga, kwa sababu waliona kitu kilichokuwa kikipinga. Nao hawakuwa na ujasiri, ha—hawakuwa na kile ambacho tungekiita leo, ne—neno la mtaani, hawakuwa na—na—na "juhudi kubwa." Kuna kitu kilichokosekana. Wasingeweza kwenda huko nje na kukabiliana na jitu hilo. Kwa nini? Lakini wote walibarikiwa na kasisi. Walikuwa na baraka takatifu juu yao, na walikuwa wamepiga magoti na labda wakapakwa mafuta kwa maji matakatifu, na chochote kilichokuwa, na pale wote walikuwa wamesimama pale. Bali upinzani ulipokuwa mkali sana, hawakuwa nao. Hapo alisimama Sauli, mwangalizi mkuu ama askofu, akisimama pale, kichwa na mabega yakiwa juu kuliko jeshi lake.

107 Ndipo akatoa changamoto, Goliathi alitoa, na kusema, "Nikimwua, basi mtatutumikia. Bali akiniua, basi tutawatumikieni." Lakini upinzani ulikuwa mkubwa sana. Alikuwa na vidole inchi kumi na nne, hiyo ingekuwa inchi ishirini na nane kuzunguka mkono wake. Angalia mkono wake ulivyokuwa! Si—sindano yake, sindano ya mfumaji, kama mkuki wake aliokuwa nao. Pia wazia jinsi kichwa chake kingekuwa

kikubwa, kingekuwa karibu kama beseni. Na kungekuwa na he—helmeti, unene wa inchi moja ama mbili, ya shaba, ikining'inia juu ya kichwa chake. Angalia silaha, vipande vya silaha kama moja ya madirisha haya ya luva, ambapo angeweza kupumua na kujisogeza, hivyo ndivyo silaha hizo zilivyofanya kazi. Huku koti kubwa la deraya likining'inia juu yake, labda likiwa na uzito wa ratili mia moja, ama ratili mia mbili, za shaba, zikining'inia juu ya kifua chake. Akiwa na—akiwa na sindano, mkuki mkononi mwake, labda wenye urefu wa futi thelathini na tano.

108 Kile adui awezacho kufanya anapowazia kwamba amekushinda nguvu! Kile anachowazia kuwa anaweza kufanya, jinsi atakavyojigamba! "Siku za miujiza zimepita. Huwezi kuepuka na kitu kama hicho."

109 Bali kukaja maskini jamaa aliyeonekana dhaifu ambaye hakuwa amepata ujuzi wowote wa kithiolojia, bali alikuwa na ujuzi kwamba Mungu alikuwa angali ni Mungu. Mungu hutimiza Neno Lake. Naye huyu hapa akaja. Ndipo Sauli akasema, "Ngoja, nita—nitakupa digrii ya kwanza ya sanaa."

110 Akaweka helmeti yake juu yake, nayo ikaenda, ikamdidimiza. Hakujua chochote kuhusu hiyo. Kasema, "Sijui chochote juu ya vitu vya namna hiyo." Kasema, "Sijui. Bali ninajua kitu kimoja, kwamba je! mnaogopa kwenda kupigana na lile jitu? Nanyi mnasimama hapa na kujiita wenyewe Kanisa la Mungu aliye hai, na kumruhusu huyo asiyeamini asiyetahiriwa kusimama hapo nje na kufanya majigambo namna hiyo?" Kasema, "Nitaenda nipambane naye!"

111 Loo, tunahitaji mtu kama huyo leo hii, mtu ambaye amekuwa na tukio!

112 Alifanya nini, maskini Daudi wa Bethlehemu alifanya nini? Alienda huko kupambana na hilo jitu. Jitu hilo likamlaani katika jina la miungu wake, miungu, wingi, akamlaani katika jina la majitu yake, au miungu wake, na akaenda huko nje na kusema, "Leo hii nitakuchukua kwa mkuki wangu na nitauning'iniza mzoga wako huko juu kwenye mti na kuwaacha ndege waule."

113 Akasema, "Unanikabili kama Mfilisti, katika jina la Mfilisti, ukiwa na silaha na mkuki, bali mimi ninakukabili katika Jina la Bwana Mungu wa Israeli." Ilikuwa ni kitu gani? Neno! Neno, "Nitakukabili kwa Neno." Kasema, "Leo hii nitakata kichwa chako kutoka mabegani mwako." Jitu hilo likacheka na kumwandama. Naye Daudi hakurudi nyuma, alimkabili, pia. Kuna mahali pamoja padogo tu, na Mungu akaelekeza jiwe lake.

114 Daudi, akiwa amekaa hapa juu kama mtoro, alikuwa akiwazia juu ya huo, jinsi ushindi huo mkuu ulivyokuwa. Ndipo hapana shaka alianza kuwaza kuhusu zaburi, jinsi ambavyo wakati mwingine huko nje milimani angekaa na kutafakari juu ya Mungu. Alisema alizifunga amri Zake juu ya m—

mhimili wa kitanda chake na vidole vyake, na popote aendapo. "Daima ninaye Bwana mbele zangu, daima, nami sitatikisika." Alimweka Mungu mbele zake. Na ushindi mkuu aliopata! Wakati alipokuwa amevuviwa sana, yeye alikuwa mtunzi wa zaburi, angeruka juu na kuchukua kalamu yake na kuziandika zaburi na kuziimba. Angeingia katika Roho, na kucheza na kucheza na kucheza katika Roho. Jinsi ambavyo angechukuliwa sana katika Roho, angecheza katika Roho kwa kuandika zaburi hizi. Na hapana shaka alizipitia zaburi mbalimbali, "Bwana ni Mchungaji wangu, sitapungukiwa chochote. Hunilaza chini katika majani mabichi," Zaburi ya 23, "Huniongoza kando ya maji matulivu. Yeye huirejesha nafsi yangu. Loo, Yeye huniongoza katika mapito ya haki kwa ajili ya Jina Lake. Pia, naam, nijapotembea kwenye bonde la kivuli cha mauti, sitaogopa uovu wowote. Wewe U pamoja nami."

115 Basi alipowazia juu ya mambo hayo, hapana shaka ilikuwa ni siku yenye joto, akashikwa na kiu, joto na kutokwa jasho. Angeweza kuangalia huko chini kwenye bonde kutoka kwenye vilele vya milima, upande wa mashariki ama upande wa magharibi, ama upande wa mashariki ndivyo ulivyo, wa mji, wakati alipoangalia huko chini na kuona ambapo Wafilisti wote huko chini, maelfu ya hao wamezunguka kote. Aliona kile kisima cha kale ambapo alinywea wakati mmoja. Loo, akaanza kuwaza juu ya asubuhi moja ambapo angechukua kondoo wake, aende nje ku—kuwalisha, angepitia karibu na kisima hiki cha kale, kwa sababu palikuwa ni mahali mashuhuri pa maji. Ndipo basi angeenda pale na angekunywa maji, na kunywa, awaache kondoo wake wanywe. Jinsi ambavyo kule Bethlehemu, ambapo aliwanywesha maji kondoo wake.

116 Hapo ndipo hasa ambapo Mungu huwanywesha kondoo Wake tena leo hii, moja kwa moja huko Bethlehemu, Ni Maji baridi matamu.

117 Akalia, "Laiti ningalipata maji kutoka kwenye kisima hicho tena!" Ninaenda kufunga sasa, sikilizeni kwa makini. "Laiti tu ningalipata maji!" Ndani yake akalia, "Laiti ningaliweza kupata maji mara nyingine zaidi kutoka kwenye kile kisima huko Bethlehemu." Shauku zake zilikuwa ni amri kwa wale waliompenda. Kumbuka, nafsi yake ilikuwa ikililia kinywaji cha yale maji. Na wale waliompenda, shauku yake ndogo zaidi ilikuwa ni amri. Tunaambiwa ya kwamba mmoja wa . . . watatu kati ya waume hao waliungana pamoja, watu mashuhuri. Mmoja aliwaua watu mia nane, peke yake. Mwingine aliruka ndani ya tundu na kumwua simba. Mmoja alichukua fimbo na kugonga mkuki kutoka mkononi mwa Mmisri, akamwua kwa mkuki wake mwenyewe, na akasimama kwenye uwanja wa dengu namna hiyo, na kuwaua watu mia tatu karibu naye. Watu mashuhuri! Walikuwa Wamataifa. Angalia walikotoka.

118 Daudi hapa ni mfano wa Kristo, Bethlehemu, maana Kristo ni Mwana wa Daudi. Huyu hapa amesimama pale, akililia kinywaji cha maji yale. Na shauku yake ilikuwa ni amri, nilisema, kwa wale waliompenda. Watatu kati ya watu hao walichomoa panga zao na walipiga vita maili kumi na tano ya watu, hadi kwenye mji ule. Huku wengine walipigana kuweka. . .Hao walikuwa ni mashujaa wa vita, hao Wafilisti, maradufu ya kimo chao, baadhi yao. Lakini walikuwa ni wanaume, shujaa, walioweza kupiga vita. Mmoja wao aliua, alisimama peke yake, na kuwaua watu mia nane moja kwa moja karibu naye, kwa siku moja. Walikuwa ni watu mashuhuri, walimtumainia Mungu. Walikuwa na imani kwa kiongozi wao. Nao walikata njia yake kote kupitia, mpaka wakati baadhi yao walipokata na huyo mwingine akachota ndoo ya maji, nao wakakata njia yao kurudi kupitia maili zingine kumi na tano ya watu, na kuyaleta hayo kwa Daudi ili aweze kuyanywa.

119 Hapa Kristo amewakilishwa hapa katika hili, Mfalme na pia Askari wa vita, kwa sababu alikata njia Yake akapita. Alivunja ngome ya adui ya mauti. Alivunja ngome za adui, ili, vema, tuweze kuwa na Uzima wa Milele, Maji ya Uzima wa Milele. Alipita hata kufikia mauti, na kuchukua mauti juu Yake Mwenyewe, akafa mauti, na kurudi ili tuweze kuwa na Uzima wa Milele. Yeye ni Mfalme na Askari wa vita pia. Sisi hatukushinda, imeshindwa tayari! Hatukushinda mauti, Yeye alitushindia mauti! Yeye ndiye Daudi wetu wa siku hii. Alishinda mauti. Mkate na Maji ya Bethlehemu.

120 Bethlehemu ilikuwa ndiyo kituo. Ninyi wanahistoria mnajua hayo, kwamba ilikuwa ndiyo kituo. Ilikuwa ni nchi mashuhuri ya ngano humo ndani, kutokana na unyunyiziaji na kadhalika. Wangekuwa na mavuno makubwa ya ngano. Na pia inayo maji yaliyo bora. Ilikuwa ni kituo cha mkate na kituo cha maji cha Palestina.

121 Basi leo hii, haijalishi ni mashirika mangapi tuliyo nayo, ni wangapi wengine wanaodaiwa kuwa ni ndugu, na, ambao, wanaweza kuwa, bado Kristo ndiye Bethlehemu ya mwaminio. Yeye ndiye mahali pa Mkate na Maji. Wamethodisti, hilo linawafaa; hilo linawafaa ninyi Baptisti, ninyi Pentekoste, ninyi wengine. Yote ni mahali pamoja, hapo ni Bethlehemu. Ndipo ambapo Mkate na Maji ya Uzima hutokea. Naam.

122 Hapa Yeye ndiye Mkate wetu, Mkate wa Mungu na Maji kwa ajili yetu. Yeye ndiye kituo, mahali pa pekee uwezapo kuja na kupata Huo, ni kutoka Kwake. Nyumba ya Mungu, katika utu wa Yesu Kristo, Bethlehemu yetu, Mkate na Maji ya Uzima wa Milele. Na Yeye ni Neno lililofanyika mwili. Hili hapa Neno, Mkate na Maji ya Uzima. Waebrania 13:8 inasema, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Hiyo inamfanya kuwa Bethlehemu yetu, mahali petu pa Mkate na Maji, mahali pa pekee pa Uzima wa Milele.

123 Mwangalie Daudi, alipoyapata hayo maji, hakuyanywa. Alisema, "Mungu anizuie. Hii ni damu ya watu hawa waliohatarisha maisha yao," kwenda na kumletea maji hayo. Angalia! Aliyamwaga juu ya nchi, kama toleo la kinywaji kwa Mungu. Amina! Wanaume na ndugu zangu, inueni imani yenu kwa dakika moja tu sasa. Alikataa kuyanywa, mwenyewe. Aliyamwaga juu ya nchi, kama sadaka ya kinywaji kwa—kwa Mungu.

124 Jinsi hiyo inavyoingiana na Yohana 3:16, wakati Mungu alipoupenda sana ulimwengu hata akamtoa Mwana Wake wa pekee. Yesu, Mfalme wa Uzima, alikuja hapa, haikumlazimu kufa. Alishinda mauti Yeye Mwenyewe, na kumwaga Damu ya Uhai Wake Mwenyewe juu ya nchi, amina, kama toleo kwa ajili ya dhambi zetu. Yeye ni mwamba wetu uliopigwa. Juu ya nchi, Damu Yake ya thamani aliyopewa na Mungu.

125 Nilimsikia mtu fulani akisema hivi majuzi usiku katika ujumbe, alisema kwamba walikuja kwenye. . . Ninaamini ilikuwa ni Billy Graham, jana usiku, nilikuwa nikimwangalia wakati aliposema kwamba alienda Israeli na akaenda Palestina, naye akasema, "Nimekuja kuwaamini watu wenu," kitu kama hicho. Na hakika nilipendezwa naye wakati alipoonekana kwenye kile kipindi cha kilimwengu jana usiku. Wengi wenu mlimkataa mtu huyo kwa kufanya hivyo. Lakini, angalieni hapa, alikuwa mbele ya taifa lote wakati huo. Wala hakulikana, alisimama hasa juu ya kile alichoamini. Nami hakika ninampenda kwa sababu ya jambo hilo. Ndipo akasema, "Nilienda Israeli nami nikawaambia, 'Mimi humwabudu mmoja wa Watoto wenu,' kwa maneno mengine, namna hii."

126 Nikawaza, "Billy, hiyo ni ya ajabu. Ningependa kuona nguvu hizo alizotoa Mungu hata inakubidi kusimama pale miongoni mwa huo umaridadi wa Hollywood na kutoa ushuhuda kwa Yesu Kristo, lakini Yeye hakuwa Myahudi." Yesu alikuwa ni Mungu, si Myahudi. Kumbukeni, seli ya damu hutoka kwa jinsia ya kiume. Na Yeye kabisa hakuwa mwanadamu, Myahudi wala Mmataifa, Yeye alikuwa ni Mungu aliyeumbwa katika mwili. Hatuokolewi kwa damu ya Myahudi wala damu ya Mmataifa, tunaokolewa kwa Damu ya Mungu. Yeye alikuwa ni Mungu, hakuna chochote pungufu. Hakuwa Myahudi wala Mtaifa. Damu umbivu ya Mungu ndani Yake, tunafanyika. . . Kama Yeye alikuwa ni Myahudi au Mtaifa, sote tumepotea. Yeye alikuwa ni Mungu katika mwili. Kweli.

127 Mimi simwabudu Myahudi, ninamwabudu Mungu ninapomwabudu Yesu Kristo. Siabudu kitu fulani cha kubuni wala kitu fulani cha kihistoria. Ninamwabudu Yesu Kristo, Uwepo wa Yesu Kristo sasa hivi, ambao ni Neno Lake lililodhihirishwa katika wakati huu.

128 Mungu katika kila wakati alitenga Neno Lake tangu mwanzo, na kila wakati ambapo mojawapo ya nyakati hizo ulipita, Mungu humtuma duniani nabii aliyepakwa mafuta kwa ajili ya wakati huo. Katika siku za Nuhu, siku za hao wengine wote, wakati Yeye alipozitoa ahadi. Sijali ni hali ya jinsi gani kanisa liliingia, Yeye daima hufanya hivyo, Yeye humtuma mtu aliyepakwa mafuta. Kwa kuwa Neno la Bwana huwajia manabii. Na hapa Yeye alisimama hapo, kila nabii, na alihukumiwa na mashirika ya siku hiyo, bali alisimama juu ya Neno na kufanya Neno liishi.

129 Yesu alikuwa ndiye utimilifu wa Neno la Mungu, kwani Yeye alikuwa ndiye utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya kimwili, na ndani Yake mlikaa utimilifu wa Mungu. Mungu aliishi ndani ya Yesu Kristo. Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. Si Myahudi wala Mtaifa, bali Mungu! Hapo Yeye alisimama, akijifanya Mwenyewe. Jinsi inavyotoshea! Na Damu ya Mungu Mwenyewe ilibidi imwagike juu ya nchi, kuanzia damu isiyo na hatia ya Habili kote kote, kutukomboa sisi. Yeye hakuutoa uhai Wake mwenyewe, hakuuzuia uhai Wake mwenyewe; Yeye alisema, "Baba, je! inawezekana kikombe hiki kiniondokee Mimi? Bali, hata hivyo, si mapenzi Yangu, Yako yafanyike." Alijisalimisha kwa Neno.

130 Leo hii tunaweza kufanya jambo lilo hilo. Unaweza ama kuchukua kanuni zako za imani, uchukue *ninii* yako, na uende popote utakapo nayo; bali unaweza kusema, "Si mapenzi yangu, bali Yako yafanyike." Rudi kwenye hilo Neno la Mungu. Yachukue mapambo yako na Krismasi na ufanye nayo kile utakacho. Bali nipe Yesu Kristo moyoni mwangu, haijalishi jinsi Hilo lilivyo duni, na jinsi watu wanavyolicheka Hilo, ama ni nini kuhusu Hilo. Angalia—angalia tabia yake, uone kama linatenda kama vile tu Yeye alivyotenda. Kama halikufanya, wala halilingani na Neno hili, achana nalo, hilo si Kristo; maana Kristo ni Neno.

131 Sasa tunaona jinsi ulivyofaa, Mwamba wetu, uliopigwa, Damu ya Uhai Wake ilimwagwa juu ya nchi, dhabihu ya dhambi kwa mwenye dhambi. Bethlehemu yetu, Maji, Mkate na Uzima, zimetolewa kwa utakaso kwa ajili yetu wenye dhambi tusio safi.

132 Loo, rafiki yangu mwenye dhambi, unawezaje kukataa, kijinga sana, toleo kama hilo, wakati Mungu alimtoa Mwana Wake wa pekee, toleo la dhambi, kwamba yeyote amwaminiye Huyo, katika Yeye, hataangamia bali atakuwa na Uzima wa Milele? Unaingiaje ndani Yake? Kwa Roho mmoja sote tunabatizwa ndani ya Bethlehemu moja, Neno la Mungu, ambalo ni Kristo aliyedhihirishwa kwa ajili ya wakati huu.

133 Na kila ahadi ambayo Biblia inatoa ya wakati huu, Yeye anamngojea nabii fulani kusimama jukwaani kudhihirisha hilo, Yeye aliahidi hilo kulingana na Malaki 4. Itafanyika.

Haijalishi jinsi watu wanavyowazia kipumbavu, itafanyika hata hivyo! Mungu alisema hivyo! Yeye anaweza kutokana na mawe haya! Kanuni zetu za imani hazitaipokea, kama makanisa yetu hayataipokea, Mungu anaweza kurudi kwenye zizi, Yeye anaweza kwenda popote atakapo. Lakini kutakuwako na mtu atakayelitetea Neno hili lililonenwa kwa ajili ya siku hii. Kitu fulani hakina budi kudhihirisha Hilo. Haitakuwa ni kikundi, hata, kamwe haikuwa.

134 Ee wanangu, askari wa vita, ninapofunga. Sitaki kuwaweka hapa kwa muda mrefu kupita kiasi. Ninaenda kufunga sasa hivi, Bwana akipenda. Bado dakika tano ifike saa tano, ama dakika sita, hasa. Tazameni, Enyi wana mashujaa, nyinyi wanaume hapa mnaodai kuwa mwana! Je! mlijua kile Daudi alichowakilisha? Daudi alimwakilisha Kristo, Yeye alikuwa, Kristo alikuwa ni Mwana wa Daudi. Sasa sikilizeni, katika kufunga. Hao askari wa vita wa Mataifa, wengi wao, angalia walikuja kutoka kila mahali, bali walijua kwamba huyo mtoro alikuwa amepakwa mafuta. Walijua kwamba Daudi alikataliwa na watu wake mwenyewe, lakini walijua kwamba upako ulikuwa juu yake. Waliweza kuuona. Kwa hiyo wakasimama moja kwa moja pamoja naye, kufa au kupona! Walikuwa watu hodari, haijalishi ni kiasi gani ulimwengu wa nje hawakuamini hilo.

135 Watu wake mwenyewe walimtupilia nje. Hawakutaka uhusiano wowote naye. Sauli alimtorosha, kiongozi wa dhehebu alimtorosha, na hana uhusiano wowote nalo, baraza lilimtupa nje, ndipo akawa mtoro. Ilimbidi kwenda popote alipoweza. Huyo hapo alikuwa juu milimani, bali kulikuwako na kundi dogo la wanaume, la Mataifa na kadhalika, lililoundwa, kwamba walimwangalia mtu huyo na wakajua alikuwa ni mfalme ajaye.

136 Ndivyo ilivyo leo hii na askari hodari wa vita vya imani ya Neno hilo, wanaojua Neno hilo linaahidi kwamba Yesu Kristo atarudi. Hatuvutiwi na mamilioni ya dola ya *hili* na mamilioni ya dola ya *lile*. Ninavutiwa na kurudi kwa Kristo Yesu. Ee askari wa vita wana wa Mungu, mna shida gani, mnasimama namna gani leo hii? Tunapoona ya kwamba Biblia inatabiri ya kwamba yeye ni mtoro leo hii, amefukuzwa kutoka kwa kanisa Lake, amefukuzwa kutoka katika mashirika. Nanyi mnajua hilo. Hamna haja ya kujificha kuhusu hilo, hilo ni kweli. Biblia ilisema ingekuwa hivyo. Ziondokeeni hizo alama za mnyama!

137 Waangalie wanaume hawa! Walichomoa panga zao. Ilikuwa ni nini? Shauku yake ilikuwa ni kinywaji cha maji baridi. Daudi! Ni mfano wa jinsi gani wa leo hii, Daudi wetu, Kristo, tunajua Yeye anaitwa mtakatifu anayejibingirisha, ametupwa upande mmoja, mlokole katika kila jambo, amekataliwa na makanisa. Wana kanuni zao za imani na mambo yaliyopangwa katika Krismasi hii kama walivyofanya kwenye ile ya kwanza. Tunajua hilo, bali tunajua kwamba Neno hili daima hubaki kuwa kweli,

Nalo halina budi kutimizwa. Na matakwa ya Kristo ni kwa wanaume, askari wa vita, kusimama! Amina!

138 Loo, njoo, simama pamoja nami, kando yangu. Ninasimama mahali pa kutisha. Ninatoa changamoto leo! Kanda hizi zinaenda kote ulimwenguni. Ninampa changamoto mwanaume fulani, askari fulani wa vita anayempenda Yesu Kristo, ambaye anajua kwamba mambo haya hayana budi kutimizwa leo hii, ndugu zangu, njoo usimame kando yangu na ulivute Neno la Mungu. Yasahau hayo mabirika yaliyokauka na madhehebu yaliyotuama mnayoishi ndani yake. Livute Neno safi la Mungu, hebu tumpe Yesu kinywaji kizuri cha Maji safi ya kipentekoste! Hiyo ndiyo shauku Yake leo hii, kurudi kwenye pentekoste ya asili, kurudi kwenye Neno! Imetabiriwa kwamba tutafanya hivyo, katika Malaki mlango wa 4, "Kurudisha Imani ya watoto kwa baba zao tena." Ni nani angaliweza kusimama asubuhi ya leo?

139 Kama vile Daudi, tunajua kwamba Daudi anakuja mamlakani. Yesu Kristo anaenda kuuteka ulimwengu. Anairithi dunia, Yeye anaenda kuwa Mfalme juu ya ulimwengu huu. Amekataliwa leo hii, Yeye ni mtoro miongoni mwa watu Wake. Bila shaka, Yeye ni mtoro kwa ulimwengu, daima amekuwa hivyo. Lakini leo hii Yeye ni mtoro kwa kanisa Lake mwenyewe, wanamkataa, wanapenda kanuni zao za imani na wakubwa wenye vyeo badala ya Neno. Hawatamwacha Yeye adhihirishwe. Hawatamwacha Yeye kuhubiriwa katika nguvu Zake. Wamejikatilia mbali na Hilo, kama tu vile Biblia ilivyosema wangefanya katika Ufunuo 17. Wanafanya nini? Wanaenda hapa juu leo hii, na wote wanaingia katika Baraza hili la Makanisa. Ukatoliki na Uprotestanti zikiungana pamoja, zikifanya alama na sura ya mnyama. Nao Waprotestanti wakiangukia hilo moja kwa moja, Wapentekoste kila mahali. Wenye vyeo wakienda Roma, kutoka Pentekoste, na kurudi, kasema, "Mahali pa kiroho zaidi!" Pia huko Texas na kila mahali pengine, wanafungua na kutoa ufahamu wa vituo na kadhalika, wakijua kwamba hizo ni kanuni za imani zilizoingizwa kwenye hili Neno.

140 Loo, enyi wakaaji wa Bethlehemu! Haleluya! Ninaitia wanaume, askari wa vita wasio na woga. Sijali kama kuna mia nane wamesimama upande mmoja na elfu kumi upande mwingine, ninataka askari wa vita ambao watakuja pamoja nami na kufanya shimo kupitia ngome hii ya Wafilisti wasioamini Baraza la Ulimwenguni limezunguka Neno la Mungu, likijaribu kulifanya kanuni za imani na kuwalisha watu. Kuna Kisima, kuna Chemichemi iliyofunguliwa katika Nyumba ya Daudi, Bethlehemu, kwa ajili ya dhambi na uchafu. Ndugu, dhambi ni kutokuamini Neno Lake!

141 Ni askari yupi anayeweza kuuona Utawala wa miaka elfu ukija? Ni askari yupi wa vita anayeweza kumwona huyu Roho

Mtakatifu mkuu akija katika umbo la Yesu Kristo, mwili halisi wa Kristo kuchukua mamlaka tena, simama pamoja nami. Simama karibu nami! Hebu tutoboe shimo katika kanuni hizi za imani ya kidhehebu. Hebu tuingie humo! Yeye analilia kinywaji kizuri cha Maji ya kipentekoste, pentekoste ya asili, si kundi la kufanya yasiyofaa, kupiga mayowe, kupiga makelele, hapa. Ninamaanisha ubatizo halisi wa Roho Mtakatifu unaofanya Uhai wa Yesu Kristo kurudi ndani ya mtu huyo.

142 Samahani kama nimewaudhi. Hapana, msifanye hivyo. Ninafanya haya katika Jina la Bwana Yesu. Rudini! Simama, ewe mwanamume shujaa unayemwona Daudi akisimama huko ng'ambo! Yesu Kristo, mtoro kutoka kwa kanisa Lake, akizuiliwa na kanuni zao za imani. Kuna Chemichemi safi inayoning'inia kule ng'ambo. Amina. Zipo nguvu za kulifanya Neno hili kuishi tena, imetabiriwa katika siku hii kuja kutimia. Mungu alisema ingekuja kutimia. Haina budi kutimia. Hutafanya hivyo katika jeshi ulilomo sasa. Umezungukwa wewe mwenyewe, Pentekoste, moja kwa moja kuzungukwa na madhehebu hayo mengine, kulikata kuwa kanuni ya imani.

143 Ee watu wa Mungu, u wapi ule Upanga? Bwana wetu anatamani maji safi. Sijali kama ni uhai au mauti, hebu tupenye kupitia kitu hiki. Ni vigumu sana kusimama peke yako. Ninaitia wanaume kusimama pamoja nami, kusimama pamoja na Neno! Kile Neno hilo lisemacho, kifanye jinsi tu Neno hilo lilivyosema. Sijali yale kitu kingine chochote kisemayo, lidumishe Hilo namna hiyo, kwa kuwa Hilo ndilo kitu pekee kitakachopenya. Hebu twendeni Bethlehemu, Maji halisi ya Mungu.

144 "Mtu akikaa ndani Yangu nami ndani yake, mkikaa ndani Yangu na Maneno yangu ndani yenu." Kudumu, si tu kuruka kutoka mahali pamoja hadi pengine, na kubadilisha kadi yako ya ushirika kutoka kwa wa umoja kwenda kwa uwili na utatu, na kurudi kwenye Presbiteri, Lutheri. "Mkikaa ndani Yangu," na Yeye ni Neno, "Maneno Yangu yakae ndani yenu! Usiogope mia nane au milioni nane. Nitasimama kando yako. Ninatamani kunywa kutoka Kisima kile tena."

145 Mungu anaenda kuwa na watu watakaokinywea Kisima hicho! Haleluya! Huenda ukadhani kwamba nina wazimu, na labda ndivyo nilivyo, basi nina wazimu kuhusu Yesu Kristo na Neno Lake. Kama inabidi niitwe mpumbavu, acha niitwe mpumbavu kwa ajili ya Neno Lake. Kamwe sijawapinga watu walio katika hayo madhehebu. Ninapinga mfumo huo ambao unalizuia Neno la Mungu. Hebu tupenye, enyi askari wa vita. Simama pamoja nasi. Hebu tuende kwenye Kisima kile. Yeye ndiye Bethlehemu yetu.

146 Mabirika haya ya kale, Baraza la Makanisa ya Ulimwenguni likiundwa sasa. Hebu turejeshe Neno safi la Mungu, si dhehebu. Hebu tusichukue kanuni ya imani, hiyo ni mabirika ya

kale yaliyotuama yaliyoshuka miaka arobaini iliyopita, miaka ishirini iliyopita, miaka thelathini iliyopita, ama pengine mwaka uliopita. Ninataka Neno la Mungu lililoahidiwa kwa ajili ya siku hii. Hicho ndicho kinywaji Yeye anachotaka niwe nacho, Neno hili leo hii! Ni Bethlehemu mdogo, imekataliwa.

147 Ni, ninajua, ni kama tu, unawazia, "Vema, kama ninii yangu . . . " Naam, hiyo ni kweli, walidhania kwamba anapaswa kuzaliwa Yerusalemu. Walidhani Yeye anapaswa kuzaliwa mahali palipo na viongozi wa dhehebu lao. Bali aliyapindua hayo yote. Alilijia jina Bethlehemu, kwa kuwa hiyo ndiyo aliyokuwa. Haleluya! Hawajii Methodisti, Baptisti, Presbiteri au Wapentekoste. Anamjia Bibi-arusi, Yesu Kristo. Huyo ndiye ambaye Yeye anamjia. Huenda likaonekana la kigeni kwako, bali amini Hilo!

148 Mnaona mifano hii? Haiwezi kuja kwa njia yoyote nyingine ila kupitia Neno. Hapo ndipo mahali pekee Yeye angaliweza kuzaliwa, ni kwa hiyo Bethlehemu. Hiyo ndiyo sababu ilibidi pawe ni mahali pale padogo panyenyekevu. Hivyo ndivyo haina budi iwe asubuhi ya leo, haina budi iwe vivyo hivyo kwa Neno lililoahidiwa. Naam, bwana. Baraza la Makanisa ya Kifilisti sasa linaundwa, limezunguka Bethlehemu yetu kote. Majira haya ya Krismasi, wamezunguka pale, kila mahali, yote imepambwa na mapambo ya ulimwenguni. "Loo, tutaleta amani ulimwenguni." Papa Luther, John, ama lolote lililo jina lake, ataleta pamoja, na maaskofu wote mashuhuri wa kanisa, Baraza la Muungano wa Makanisa na Baraza la Ulimwenguni yote yakiungana pamoja. Wawili wanawezaje kutembea pamoja wasipopatana? Amina!

149 Yupo Mmoja tu unayeweza kutembea naye, huyo ni Yesu Kristo. U—unawezaje kutembea pamoja na Yeye? Ukikubaliana na Yule Yeye aliye, Neno! Usiache hilo likuondokee.

150 Sijali ni kiasi gani cha mapambo waliyo nayo, "Huna budi kufanya *hili* ama tutafunga kanisa lako ulilo nalo." Sijali kile wanachofunga, na haina uhusiano wowote na Neno. Naam, bwana. Unaenda wapi? Kile hasa Neno lilichosema ulikuwa unafanya, kurudi moja kwa moja, wote wamevikwa na mapambo ya ulimwengu, pamoja na namna zote za ahadi za kilimwengu, bali ni mbali na Neno maili milioni moja. Hiyo hapo leo hii, Krismasi tena, kutuweka mbali na ahadi ya Neno. Lakini Hilo litatimizwa. Mungu anaweza kutokana na mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto. A-ha, kujaribu kuwaweka wakaaji halisi, wa Bethlehemu mbali na Uzima wa Milele, hilo ndilo lengo lao.

151 Amkeni, enyi wana na askari wa vita, hebu tupenye kurudi kwenye Bethlehemu yetu ya asili! Kumbukeni wakati Daudi alipokuja kwenye enzi yake. Watu hawa walisimama naye kwa sababu alijua, walijua alikuwa anakuja mamlakani. Walijua kwamba Daudi alikuwa anaenda kuwa mamlakani, haijalishi

jinsi alivyokataliwa. Alikuwa ndiye mtoro mbaya kabisa nchini. Na ndivyo ilivyo na Neno la Mungu, asubuhi ya leo, Hilo ni geni kwa madhehebu. Angalia walichofanya. Hiyo inalionyesha moja kwa moja mbele yenu.

152 Watu wanajaribu kusema, "Ndugu Branham, unaligonga kanisa." Ninagonga mifumo hiyo. Kanisa ni Yesu Kristo, si mfumo.

153 Basi leo hii, angalia kile walichofanya, angalia kile wanachofanya. Ndipo unaweza kuona kile wanachofanya, wanajaribu kuwaweka watu mbali na Hilo. Wanazunguka na kuzunguka zaidi kwenye hicho Kisima, ili kuhakikisha kuwa hakuna mtu atakayekunywa kutoka kwa Hicho. Bali, Ee askari wa vita wa Mungu, ninaamini kwamba Yesu Kristo atakuja siku moja katika utukufu, ninaamini Yeye atakuja na kuketi kwenye Enzi ya Baba Yake Daudi. Ijapokuwa Yeye ni mtoro, Neno Lake asubuhi ya leo, amekataliwa na watu Wake Mwenyewe kama Daudi alivyokuwa, madhehebu yalilikataa Neno Lake, walilitupilia nje, wakati Mungu anapokuja na kulithibitisha Neno Lake safi. Usiniambie! Kwa miaka, kote nchini, nao wanaenda mbali zaidi, mbali na Hilo wakati wote.

154 Nilisema hivi majuzi, kuhusu Jacqueline Kennedy, mara ngapi nimewakemea enyi wanawake kwa kukata nywele zenu, kujipodoa, enyi wanawake wa Kipentekoste mnakata nywele zenu, ambalo Mungu alisema ni . . . u—u—unajifanya mwenyewe ka—kahaba wa mtaani wakati unapofanya hivyo. Na, kulingana na Mungu, mume wako hana haki ya kuishi na wewe zaidi. Mwanamke anayekata nywele zake, anaaibisha kichwa chake, ambacho ni mume wake. Hiyo ni hakika. Ninasema nini kuhusu hiyo? Na nyinyi mnanipigia simu kuihusu, ninapokea barua, "Wewe mzee wa ajabu." Vema, walimwita Eliya vivyo hivyo. Waliliita kila Neno la Mungu, kila mara Neno linapofanywa, wanaita Hilo.

155 Mtu fulani alisema hivi majuzi, "Mbona, tunakuamini wewe kuwa ni nabii."

156 Kamwe sikusema hilo, sisemi. Mimi si nabii, mimi ni mtumishi tu wa Mungu hapa nikijaribu kuwaambia Kweli. Hivyo tu. Hebu niwaambieni, Neno la Mungu linatetea hilo! Yeye alisema, "Mabinti wa Sayuni, tawi lililoponyoka katika siku ile ya kuchafuka kwake kwote, litakuwa lenye utukufu machoni pa Bwana." Penyeni mpite, enyi wanawake, mnapo mahali penu pa kupenya na kupitia, Hollywood ya kilimwengu na sinema, na takataka hizi zote za televisheni mnazojaribu kuiga, mkivalia kizinifu mtaani.

157 Ndipo mtu fulani akasema, "Mbona, watu wanataka uwafundishe jinsi ya kupokea Roho Mtakatifu na jinsi ya kupata . . . "

158 Unasema kwamba una Roho Mtakatifu, na kisha ukane Neno? Maisha yako yenyewe yanathibitisha kwamba huna Huyo. Mnaona? Sasa, sijakasirika, ninawaambieni tu kilicho Kweli. Jichunguze uone. Paulo alisema, "Kama malaika kutoka Mbinguni alifundisha chochote tofauti, na alaaniwe," Wagalatia 1:8. Hiyo ni kweli.

159 Vipi kama Jacqueline Kennedy. . . Aliongoza mwendo wa wanawake pamoja na mitindo hii yote ya kukata nywele kichwamaji na mambo waliyo nayo, mavazi haya yote ya kizinifu, na kama mavazi ya kina mama na kadhalika. Kila mwanamke nchini anataka kuvaa hizo, enyi Wapentekoste, pia. Angalia, Jacqueline Kennedy hakuwahi kusikia Ujumbe kama huu. Kama angesikia Huo, huenda angekuwa ametubu muda mrefu uliopita. Lakini nyinyi wanawake wa Kipentekoste mnasikia Huo, siku baada ya siku, na mwaka baada ya mwaka, na bado hamfanyi lolote juu yake! Haleluya! Mungu anaenda kuchoka moja ya siku hizi! Mungu atachoka. Vema, ninajua mnawazia kuwa nina wazimu. Endeleeni, ni sawa. Waliwazia hivyo kote katika nyakati wakati Neno . . . Mnaona?

160 Ee askari wa vita, chomoeni huo Upanga, hebu tutetee kila kitu Upanga huo unachotetea! Hebu twendeni kwenye Kisima kile palipo na Chemichemi iliyojaa Damu, iliyotolewa kwenye vena za Imanueli. Si Myahudi. Vena za Imanueli, Mungu pamoja nasi, ambapo wenye dhambi wakizamishwa chini ya gharika hupoteza mawaa yao yote ya dhambi.

161 "Ndipo atatokea Mtawala kutoka Bethlehemu ambaye atawatawala watu Wangu." Roho Mtakatifu leo hii huwatawala watu, na Roho Mtakatifu ni Neno. Je! hiyo ni kweli? Sasa, katika kufunga, kwa kicho. Yeye huwatawala watu. Haijalishi kile unachowazia; wewe ambatana na Neno. Usipofanya hivyo, Roho Mtakatifu hayupo hapo; unashuhudia ushuhuda wako mwenyewe, haijalishi yale usemayo. Ungeweza kuruka juu-chini, unene katika ndimi, na kukimbia kote sakafuni, ungali una nywele zilizokatwa na kufanya mambo unayofanya; inashuhudia dhidi yako, kwamba sivyo ilivyo.

162 Wakaaji wa Bethlehemu, Mungu awabariki, hebu tupenye! Kristo anataka Kanisa halisi. Anataka Bibi-arusi. Hebu tujikatie njia zetu za kupenya. Tuondoke mahali hapa, tuziondolee mbali hizi kanuni za imani, ili wanywaji halisi waweze kurudi na kupata kinywaji halisi, cha Maji baridi ya kipentekoste ambayo yalibubujika wakati mmoja kutoka kwenye Kisima hiki mashuhuri. Yangali yanabubujika. Hivi hutakuja leo hii na kuamini hilo kwa moyo wako wote, wakati tukiinamisha kichwa chetu kwa muda mfupi tu.

163 Ninayo mambo mengi hapa ninayopaswa kuzungumzia. Muda hautaruhusu, ni saa tano sasa. Sijui ni askari wangapi wa vita humu ndani, enyi wahudumu, Methodisti, Baptisti,

Presbiteri, kasisi wa Katoliki, chochote uwezacho kuwa, je! umeshawishika? Ninajua mimi si kasisi. Huenda nimekuja kutoka nyikani, nikiwa na *hiki* kilichokatwa, *kile*, na *kinginecho*, bali Hili ni Neno. Nanyi mnaamini Hili kuwa ndilo, na mnaamini kuwa Hili ni Neno, ambalo ndilo Bethlehemu. Yesu alisema, "Mtu hataishi kwa mkate pekee; kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Nalo Neno lipo hapa, Biblia. Mtu ataishi kwa Hilo, na Yeye ni hilo Neno.

164 Ee askari wa vita, hivi utachomoa Upanga wa Mungu na kusema, "Nimemalizana na haya mapokeo, ninarudi kwenye Neno, ninarudi kwenye Kweli"? Wanawake, wanaume! Wanawake, hamjionei aibu, jinsi mmekuwa mkifanya? Je! mko tayari asubuhi ya leo, kwenye Krismasi hii, kurudi na kumwakisi Yesu Kristo halisi?

165 Sasa huku vichwa vyenu vimeinamishwa na kila jicho kufumbwa, je! waweza kuinua mkono wako, useme, "Omba, Ndugu Branham. Kwa kweli ninataka kufanya hivyo moyoni mwangu. Mimi, ninaamini hilo"? Mungu awabariki. Jamani, wahudumu, wanawake, kila mahali!

166 Katika Bethlehemu, Bethlehemu, mahali pa Mkate na Maji ya Mungu, Kristo Bethlehemu yetu tukufu. Tunaingiaje ndani Yake? Wakorintho wa Kwanza 15, "Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa katika Mwili wa siri wa Yesu Kristo."

167 Tunakula Neno Lake, si kitu chochote kingine, Chakula cha kondoo pekee! Hilo Neno! Si kitu chochote kingine. Huwezi kuweka kanuni yoyote ya imani ndani ya Hilo, hatutaisikiliza. La, bwana. Unaenda kusema, "Mbona, liko *hivi*." Kama Biblia inasema liko Hivi, Hii ndiyo njia tunayolitaka Hilo. Hatutaki Hilo likiwa limetiwa chumvi. Tunalitaka tu jinsi Hilo lilivyo.

168 Ee Mungu, Baba yetu, leo hii ipo mioyo yenye njaa ingali imeachwa duniani. Kwa nini Bethlehemu mdogo. Katika njia yangu duni bila elimu, Bwana, nimejaribu kulifanya kundi hili dogo . . . linalonipenda, ninajua wananipenda, Bwana. Nami ninawapenda. Nami ninawapenda sana hata, Bwana, ni—nina juhudi kuwahusu. Sitaki kuwaona wakichangamana katika vitu hivi mashuhuri, na kutengwa wakati huo kukiwa kumechelewa kupita kiasi, na kuziona maskini nafsi hizo huko gerezani, na kujua wakati mmoja walikuwa na fursa.

169 Bwana Mungu, leo hii, haijalishi Yerusalemu kuu inawaza nini, na kile Gileadi na Ramoth-Gileadi na chochote kile, Shilo, na mahali mashuhuri pa ibada, popote pale. Kuna Bethlehemu. "Hu mdogo kuliko wote miongoni mwao? Bali kutoka kwako!" Kutoka nje ya Methodisti, Baptisti, Presbiteri; Katoliki, mji mkuu; na Ramoth-Gileadi, ambapo Luther alipiga vita; na—na Shi—Shilo, ambapo labda Wesley alipiga vita; na—na sehemu zingine nyingi. Lakini, Bwana, Bwana, Wewe uliinua kundi la

Pentekoste, na kama hawajageuka moja kwa moja na kufanya jambo lile lile!

170 Yesu wa Nazareti, ninakuomba Wewe, Bwana, kuwaruhusu askari wa vita, kutoka kwenye kila moja ya kanuni hizi za imani huko nyuma, wainuke katika Jina Lako, wapenye kupitia kanuni hizi zote za imani na kurudi kwenye Neno la kweli, lisiloghoshiwa, wakiweka kando kila mzigo uwazingao kwa urahisi, wakiweka kando kila saa wanayokuwa hapa nje wakiteremka kipumbavu wakijaribu kufanya washiriki wa dhehebu. Bwana Mungu, jalia warudi watafute waongofu kwa Yesu Kristo; si kutukuza dhehebu lolote ama watu wowote, ila Yesu Kristo, Yeye pekee.

171 Ilikuwa ni Daudi ambaye wale watu walimpigania. Ilikuwa ni Daudi waliyemwekea maisha yao hatarini. Na hao askari mashuhuri wa vita, bila woga, walipenya kupitia pale, kwa kuwa ilikuwa ni shauku yake. Ilikuwa ni shauku yake kunywa maji kutoka kwenye kile kisima.

172 Bwana Mungu, labda hatujihisi hivyo, ule mvuto tu, bali, tazama, ni shauku Yako kwamba mambo haya yafanyike. Kama vile Wewe ulivyomwambia Yohana, "Hivi inatupasa sisi, ama inafaa, kwamba tutimize haki yote."

173 Inatupasa sisi, kama wahudumu leo hii, kuona ya kwamba Neno hili limehubiriwa, kuona kwamba limefanywa. Inatupasa sisi, watu wa majira haya tunayoishi. Watu mashuhuri duniani leo, Ee Mungu, wako huko nje, jalia waone hilo na kunyakua Upanga! Haijalishi ni nini pingamizi, kama Mungu yu upande wako, ni nani awezaye kukupinga? Hatujali, kuweka hatarini maisha yetu ya kijamii. Hatujali, kuweka hatarini *hiki*, *kile*, au *kinginecho*. Tunataka kurudisha Maji ya Uzima!

174 Tujalie kwenda Bethlehemu, Bwana, jalia kila mmoja wao. Wajalie wanawake hawa wote, ambao, hakika, kama wakiinua mkono wao, walijionea aibu. Jalia watambue kwamba wanaume hawa watakuwa kama Bw. Kennedy moja ya siku hizi. Wata—watakuwa kama wanadamu wengine, hawana budi kufa. Wanawake hawa wanakufa. Mimi ninakufa. Sisi sote tunaungua hapa duniani, na tunajua kwamba muda mfupi tu, tunazo siku chache tu zilizosalia. Na, Mungu, badala ya kujaribu kujenga mifumo mikubwa, Bwana, jalia wanaume na wanawake waone asubuhi ya leo ni kuja kwa Mfalme.

175 Ee Mungu, kuja kwa yule Mfalme mkuu, Yesu! Na hiyo... Nasi tunatambua, Mungu, kwamba kila mmoja wa wanaume wale walioshika ule upanga na kumpigania Daudi wakati alipokuwa mtoro, wakati alipoingia mamlakani, aliwafanya viongozi wa miji. Kila mmoja wao alikuwa na miji. Na Wewe uliahidi hiyo katika Biblia, kwamba tutakuwa na miji. Ee Mungu, kama Wamataifa, walikuwa warithi kupitia Mataifa, kusudi tuwe washiriki wa utakatifu Wake na haki Yake! Tujalie

leo hii, Bwana, kama wanaume askari wa vita, tulitwae Neno hilo, tukijua kwamba, wale watakaomtetea katika majira haya, watakuwa viongozi juu ya miji. Si kwamba tunataka kuwa watawala, bali tunataka kuwa watumishi Wako, Bwana. Ee Mungu, tunaona ono la hawa wachache, kundi hili dogo, hili linaloitwa "ulokole" katika ninii. . . Paulo alisema katika siku yake, "Katika njia inayoitwa 'uzushi,'" wendawazimu. Hapo ndipo ninapotaka kupiga vita, Bwana. Neno Lako ni Kweli! Na Wewe ni Neno, yeye yule jana, leo, na hata milele.

176 Ee Mungu, tupake na Neno Lako, na kulifanya Neno Lako lililoahidiwa kwa siku hii kutimia. Jalia tutoke kwenye jengo hili asubuhi ya leo kama vyombo vya Mungu vinavyoangaza. Jalia tuenende na Upanga, Huo ukimetameta hewani, tukatilie mbali kila mzigo na kila kitu kingine, mpaka tunaweza kuwarudisha watu kwa Kristo, na kumletea Bwana wetu maji safi baridi, badala ya maskini kanuni hizi zilizotuama. Jalia watu wanywe kutoka kwenye Chemichemi, Baraka halisi ya Kipentekoste, baridi na mpya, hata iweze kubariki moyo Wake na kumrudisha miongoni mwetu tena. Tujalie, Bwana. Katika Jina la Yesu, ninaomba.

177 Huku tumeinamisha vichwa vyetu, kama mpiga piano au mpiga kinanda, ama chochote kile, ataenda kwenye kinanda, piano, ninataka kwa utulivu tuimbe huu, "Kuna chemichemi iliyojaa damu, iliyotoka kwenye vena za Imanueli; wakati wenye dhambi wakizamishwa chini ya gharika hilo . . . " Mwenye dhambi, mwenye dhambi ni kitu gani? Asiyeamini. "Wasioamini wakitumbukia." Kutokuamini nini? Neno. Loo, wale Wayahudi hawakutaka kuamini kwamba walikuwa wasioamini, walidhani waliokoka, bali Mungu alijua walihitaji Mwokozi. Walikuwa wanaombea askari wa vita, Mungu akawapa Mtoto mchanga, Mwokozi. Alijua walichohitaji. Hiyo ndiyo zawadi yao ya Krismasi. Hiyo ndiyo mnayohitaji leo, hiyo ndiyo ninayohitaji leo, Mwokozi kwa ajili ya kutokuamini kwangu, Mwokozi kutoka kwa kutokuamini kwako. Huku tukiimba, hebu tuombee tu jambo hilo sasa mioyoni mwetu. Omba tu kwa uaminifu, tafadhalini, kanisa.

> Kuna chemichemi iliyojaa damu,
> Iliyotoka kwenye vena ya Imanueli,
> Nao wenye dhambi (wasioamini) wakitumbukia (si mshiriki wa kanisa, sasa) chini ya . . . (hapo ndipo washiriki wa kanisa hutumbukia)
> Hupoteza waa lao lote la dhambi.
> Hupoteza waa lao lote la dhambi,
> Hupoteza waa lao lote la dhambi;
> Na mwenye dhambi . . .

178 Bwana Yesu, ninaomba sasa ya kwamba Wewe utatupokea. Ninajiweka mwenyewe papa hapa pamoja na kundi hili,

Bwana. Ondolea mbali kutokuamini kwangu kote, Bwana, kutoka kwangu. Jalia nife, Bwana, kama Samsoni alivyolia, jalia nife na hawa Wafilisti. Jalia nifanye lolote lile linipasalo kufanya, bali, Mungu, isafishe nafsi yangu. Ondolea mbali shaka lote. Kama kuna chochote katika Neno hili ambacho siamini, Bwana, na kama—kama hakuna kitu hapa ambacho Wewe umeahidi, ambacho siwezi kuyaona maisha yangu mwenyewe yakithibitisha hilo Neno kwa ajili ya siku hii, basi, Bwana, nisamehe. Nisamehe, Bwana.

179 Nipe ujasiri. Ee Bwana, ninahitaji ujasiri kukata na kuangusha kitu hiki, kuubomoa ukuta huu, kwa kuwa ninajua ni shauku Yako. Wewe umelinena, linapaswa kuwa katika siku hii, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Tunaona huduma hii ya mwisho, ishara hii ya mwisho iliyokabidhiwa kanisa. Hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya mwisho ya uzao wa kimwili wa Ibrahimu uliyoona kabla ya moto kuuteketeza ulimwengu wa Mataifa. Na vivyo hivyo ndiyo ishara ya mwisho ambayo Uzao Wake wa kifalme utaona kabla ya moto kuuteketeza ulimwengu wa Mataifa. Wewe. . .Bwana, jalia waone hiyo ndiyo sababu hasa iliyobidi Yesu kuzaliwa Bethlehemu. Ni Neno Lako. Ni ahadi Yako. Wabariki sasa, Baba. Ninawakabidhi Kwako, kama kumbukumbu. Pia jalia sisi, pamoja, Bwana, tulivute Neno leo hii, na tusonge mbele taratibu katika Jina la Yesu. Amina.

180 Mungu awabariki. Je! mnampenda Bwana Yesu? Je! mnaamini kwamba hiyo ndiyo Kweli? Inueni mikono yenu kama mnaamini kwamba ni Kweli. Asanteni, marafiki. Tazama, mimi. . .Nadhani kanda imezimwa. Mnaona, katika kuzungumza hapa, siwazungumzii tu nyinyi. Kanda hiyo huenda kote ulimwenguni, na wanaume na wanawake kote ulimwenguni husikia Hiyo. Tunaenda taifa baada ya taifa baada ya taifa, wananinii tu, wanaketi hapo na tyubu ndogo ndogo masikioni mwao na—na kunena Hiyo moja kwa moja kwa mamia na mamia ya watu kote ulimwenguni.

181 Na kujua, hiyo si. . .Sasa, enyi wanawake, sitaki kuudhi hisia zenu wakati nikiwaambieni hayo mambo. Lakini kama mchungaji wenu hawaambii Hilo, ana kasoro fulani. Hana—hana ujasiri wa kufanya hivyo. Anajificha nyuma ya dhehebu. Ama yeye ni kama Lutu, anaketi chini, kabla ya moto kushuka, yeye—yeye kabisa hakuwa na ki—kitu halisi kilichohitajika kusimama pale nje. Yeye. . .Biblia ilisema kwamba, "Dhambi za Sodoma ziliitesa nafsi yake yenye haki kila siku." Nafsi yake ilijua vema zaidi, bali hakuwa na kitu halisi kilichohitajika kusimama pale nje na kuikemea. Naye mchungaji ambaye hatamwambia mwanamke kwamba ni kosa kunyoa nywele zake, kuna jambo lililo kasoro na mtu huyo, na kuvaa mavazi haya.

182 Nanyi wanaume, nyinyi wanaume mtakaowaacha wanawake wenu kufanya mambo kama hayo, mna shida gani? Mna shida

gani? Unamwongoza mke wako mwenyewe kupitia mjini kama kahaba wa umma, halafu unampiga mwanamume fulani kofi mdomoni kama angemtukana. Wewe ndiwe unayehitaji kupigwa kofi mdomoni. Hiyo ni kweli, na Mungu ataifanya siku moja, pia. Hiyo ni kweli. Tunahitaji kurudi kwenye Neno hili.

183 Si hilo tu, hilo ni jambo dogo, dogo tu. Bali utayapataje mambo makubwa kama ukiyakataa madogo? Unawezaje kujifunza aljebra kama hujui ABC? Huwezi kuhesabu mpaka kumi, utajuaje hisabati yako? Inakubidi kuanzia chini. Unajaribu kuanzia kileleni, shuka hapa chini na uanze vizuri.

184 Huu ndio wakati wa kufanya hivyo, sasa, Krismasi. Ilikuwa ni kuzaliwa kwa Kristo, jalia Kristo azaliwe ndani yetu. Kristo ni nini? Kristo ni Neno. Ni wangapi wanajua hilo? "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu."

185 Mtu fulani alisema hivi majuzi, kasema, "Ndugu Branham, wewe, watu wanajua kwamba wewe ni mchukia wanawake." Sivyo nilivyo. Sivyo nilivyo. Ninao upendo halisi kwa dada zangu. Baadhi ya wanaume watageuka, wadhanie unaonekana mzuri ukiwa na macho mekundu na macho ya kijani kibichi, na nywele zilizokatwa, mwanamume huyo analo wazo tofauti na lile nililo nalo. Ninii yako . . . Ninaipenda nafsi hiyo iliyo ndani yako, ambayo inapaswa kukutana na Mungu. Hilo ndilo nina . . . dada yangu kwa ajili ya Umilele, si maskini jambo la kujuana kimwili hapa duniani litaninii . . .

186 Ni wangapi waliwahi kusoma kuzorota, kuhusu kuporomoka kwa Rumi? Hakika. Angalia pale, kitu kile kile tu tunachofanya, kuvutia kingono. Vijana katika hali ilivyo, jinsi hasa tulivyo sasa, matatizo ya kijamii. Na vijana wakichukua mamlaka, na wanaume na ngono. Jinsi tu Himaya ya Kirumi ilivyoanguka, miaka elfu moja mia nane iliyopita, nayo hii hapa moja kwa moja tena miongoni mwa Mataifa. Unaona? Machafuko miongoni mwa dini na kadhalika. Loo, ni saa ya jinsi gani tunayoishi!

187 [Dada fulani anatoa ujumbe. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Amina. Bwana Mungu amenena. Ninaamini hilo.

188 Sasa hebu tusimame. Wakati anaponena, ni wakati wetu kutoa heshima. [Mtu fulani anaongea na Ndugu Branham—Mh.] Unasemaje?

Kwa neema ya Mungu, na kwa msaada wa Mungu, nina juhudi zaidi kuliko nilivyowahi kuwa, kusimama na Neno hili na kujaribu niwezavyo, kwa msaada wa Mungu, kuikata njia kupenya kuingia Bethlehemu tena, ambapo wakaaji wa Bethlehemu wanaweza kuinywea Chemichemi hiyo. Ni wangapi watakaoungana nami, huku mikono yenu ikiwa imeinuliwa, useme, "Ninamwahidi Mungu nitafanya hivyo"? Mungu awabariki.

189 Sasa inamisheni vichwa vyenu kwa muda mfupi tu, nami ninaamini ndugu fulani hapa, Ndugu Jeffries, njoo hapa. Atawaruhusu wasikilizaji kufumukana huku tukiinamisha vichwa vyetu katika maombi, kama mtaweza. Vema, ndugu.

*Kwa Nini Bethlehemu Mdogo* SWA63-1214
(Why Little Bethlehem)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi asubuhi, tarehe 14 Desemba, 1963, kwa ajili ya kiamshakinywa cha Ushirika wa Kimataifa wa Wafanyabiashara wa Full Gospel katika Hoteli ya Ramada kule Phoenix, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2019 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


Voice Of God Recordings

P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.

www.branham.org